**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA, MHESHIMIWA CHARLES N. KEENJA (MB.), KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2005/2006.**

## UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi inayohusu Wizara ya Kilimo na Chakula na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja, kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa 2005/2006.

**2. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005 tulipata misiba ya Wabunge wenzetu wanne. Wabunge hao ni Mhe. Hayati Capt.Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Mhe. Hayati Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Mhe. Hayati Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Mhe. Hayati Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Tunawapa pole wafiwa wote na kwa kuwa wote walitokana na Chama cha Mapinduzi, nakipa Chama cha Mapinduzi pole kwa kuondokewa na wawakilishi wake. Namuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi, Amina.

**3. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kukamilisha mchakato wa kidemokrasia wa kuteua wagombea wake wa Urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2005. Utaratibu wa kuwapata wagombea Urais wa Chama cha Mapinduzi umesifiwa sana na wananchi na wageni waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Chama cha

Mapinduzi uliofanyika Chimwaga hapa Dodoma, tarehe 4 Mei, 2005. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mbunge mwenzetu kwa kuteuliwa na CCM kuwa mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama hicho. Mheshimiwa Kikwete anakubalika sana kwa makundi yote na hata kwa wapinzani kutokana na sifa bora za uongozi alizonazo. Nampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza kwa tiketi ya CCM.

**4.** Nampongeza sana Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea nafasi ya Urais wa Zanzibar. Mafanikio makubwa aliyopata katika kipindi chake cha kwanza cha miaka mitano ya Urais wa Zanzibar yanamuweka katika nafasi nzuri ya kuchaguliwa kwa kipindi cha pili kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawatakia wote ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2005 na mafanikio makubwa ya kuliongoza Taifa letu baada ya uchaguzi huo. Aidha, nawapongeza wote walioteuliwa na vyama vya upinzani kuwania nafasi za Urais katika Taifa letu.

**5.** **Mheshimiwa Spika**, naishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi kwa ushirikiano wake na Wizara ya Kilimo na Chakula katika kipindi cha miaka mitatu tangu ilipoteuliwa. Katika kipindi hicho, Kamati hiyo imetembelea maeneo mengi ya nchi, hususan maeneo ya uzalishaji, utafiti na usindikaji wa mazao ya kilimo na kutoa ushauri na maelekezo ambayo yamechangia katika kuharakisha maendeleo ya sekta ya kilimo. Katika mwaka wa 2004/2005 wajumbe wa Kamati hiyo walifanya ziara ya mikoa ya Lindi na Mtwara ambayo iliwawezesha kutembelea Kituo cha Utafiti cha Naliendele,

Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Nyangao, vituo vya kununulia korosho, kikundi cha wabanguaji wadogo wa korosho cha Tumaini na viwanda vya korosho vya Newala I na II. Aidha, katika ziara hiyo wajumbe walikutana na watafiti, wakulima na wabanguaji wa korosho na kutoa ushauri na maelekezo ya kuimarisha uzalishaji na usindikaji wa zao hilo nchini.

**6.** Naishukuru Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kupokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka wa 2004/2005 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa 2005/2006 katika kikao chake kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 2 Juni, 2005. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika makisio haya.

**7.** **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mhe. Profesa Pius Mbawala, Mbunge wa Namtumbo; Katibu Mkuu, Bw. Wilfred Ngirwa; Wakuu wa Idara, Taasisi na Asasi zilizoko chini ya Wizara; watumishi wote na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri ulioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka wa 2004/2005 na katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kilimo wa mwaka 2004/2005 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2000. Watendaji wote wa Wizara wamefanya kazi zao kwa uadilifu mkubwa ambao unathibitishwa na mafanikio yanayoanza kuonekana katika sekta ya kilimo. Nawashukuru kwa ushirikiano wao katika kuandaa hotuba hii.

**8.** **Mheshimiwa Spika**, ninawapongeza Waziri Mkuu, Mhe. Frederick Tluway Sumaye (Mb.), Waziri wa Fedha, Mhe. Basil Pesambili Mramba (Mb.), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Mhe. Dkt.

Abdallah Omar Kigoda (Mb.) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Brig. Jen. Mstaafu, Hassan Ngwilizi (Mb.) kwa hotuba zao nzuri ambazo zimechambua na kufafanua masuala mengi ya kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na hali ya kilimo na chakula nchini na hatua zinazochukuliwa na Serikali kukifanya kilimo kiwe bora na kikue kwa kasi kubwa zaidi. Wakati wa kujadili hotuba hizo, Waheshimiwa Wabunge walitoa maoni na ushauri ambao tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa uelewa wao wa sekta ya kilimo na kwa ushirikiano wao katika kuhimiza shughuli mbalimbali ambazo zimewezesha ukuaji wa sekta hiyo.

**9.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005 viongozi wetu wa Kitaifa walishiriki katika shughuli mbalimbali zinazohusu kilimo. Tarehe 11 Novemba, 2004, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Benjamin William Mkapa, alizindua rasmi kiwanda cha sukari cha Kagera baada ya shamba na kiwanda hicho kufanyiwa ukarabati mkubwa na mwekezaji. Aidha, tarehe 16 Oktoba mwaka wa 2004, Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Ali Hassan Mwinyi, alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika kitaifa katika kijiji cha Malinzanga, Iringa Vijijini. Katika hotuba yake, kwenye maadhimisho hayo, Rais Mstaafu alisisitiza umuhimu wa kilimo endelevu cha mazao ya chakula kinachozingatia utunzaji wa mazingira. Napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi hao kwa mchango wao katika kuleta mapinduzi ya kilimo nchini.

**10.** **Mheshimiwa Spika**, sherehe za Nane Nane zinazofanywa kila mwaka zimekuwa na mafanikio na mvuto mkubwa sana kwa wananchi. *S*herehe hizo zimeendelea kupanuka na kutoa fursa kwa wakulima wengi nchini kujifunza

mbinu za kilimo bora na cha kibiashara. Katika mwaka wa 2004 sherehe hizo zilifanyika kitaifa kwa mara ya pili mfululizo na kwa mafanikio makubwa katika viwanja vya John Mwakangale vilivyoko Uyole katika Manispaa ya Mbeya. Aidha, sherehe hizo ziliendelea kufanyika katika viwanja vya Themi, Arusha; Julius K. Nyerere, Morogoro; Kaitaba, Bukoba; Ipuli, Tabora; Ngongo, Lindi; Pansiansi, Mwanza; Mvumi Misheni, Dodoma; Kakonko, Kibondo na Sirari, Tarime. Maeneo mengine ambako sherehe hizo zilifanyika yalikuwa Singida Mjini na wilaya za Newala na Bariadi. Napenda kuwashukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Spika wa Bunge la Muungano, Mhe. Pius Msekwa, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Pandu Ameir Kificho, Waziri wa Ushirika na Masoko, Mhe. Clement George Kahama (Mb.) na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mhe. Edward Lowasa (Mb.), kwa kushiriki katika sherehe hizo na kutoa hotuba zilizohimiza maendeleo ya kilimo na hifadhi ya mazingira. Aidha, nawashukuru wote walioshiriki katika maonyesho ya sherehe hizo zilizofanyika katika ngazi mbalimbali hapa nchini.

**11.** Kutokana na manufaa ya maadhimisho ya sherehe za Nane Nane kwa wakulima, wafugaji na wanaushirika, napenda kutoa wito kwa Mikoa, Wilaya na Vijiji vyote hapa nchini, kujiwekea utaratibu wa kufanya sherehe hizo kila mwaka kwa kutumia rasilimali walizonazo. Kwa mfano, siyo lazima kujenga mabanda ya gharama kubwa. Serikali itaendelea kuratibu sherehe hizo katika ngazi zote. Mwaka wa 2005 sherehe hizo zitafanyika kitaifa mkoani Mbeya kwa mara ya tatu.

## HALI YA KILIMO NCHINI KUANZIA MWAKA 1994/1995 HADI 2004/2005 NA TAARIFA YA UTEKELEZAJI KUANZIA MWAKA WA 2000/2001 HADI 2004/2005

### Ukuaji wa Sekta ya Kilimo

**12.** **Mheshimiwa Spika,** kati ya mwaka wa 1994/1995 na 2004/2005 sekta ya kilimo ilikua kutoka asilimia 2.1 katika mwaka wa 1994 hadi asilimia 6.0 katika mwaka wa 2004. Sekta ndogo ya mazao ilikua kutoka asilimia 2.2 hadi asilimia 6.2 katika kipindi hicho. Kukua huko kwa sekta ya kilimo, hususan sekta ndogo ya mazao, kulitokana na hatua za makusudi zilizochukuliwa na Serikali zilizokuwa na lengo la kuondoa vikwazo vilivyofanya kilimo kidumae. Hatua hizo zimefafanuliwa katika maeneo mbalimbali ya hotuba hii.

**13.** **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha 2001 – 2005, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitekeleza **Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2000**. Ilani hiyo inaielekeza Serikali kuongeza tija katika kilimo kwa kutumia mbinu bora za kilimo, ikiwa ni pamoja na kuongeza matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo, zikiwemo majembe na mikokoteni ya kukokotwa na wanyamakazi, matrekta na mashine za kukoboa na kusaga. Aidha, Ilani ilielekeza Serikali kuendeleza kwa nguvu zaidi na kasi mpya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mwafaka kama mkakati maalum wa kujitosheleza kwa chakula na pia kutoa msukumo katika mazao mapya, yakiwemo maua, mboga, matunda na viungo.

### Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

**14. Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa mazao ya chakula uliongezeka kutoka tani milioni 7.7 mwaka wa 1994/1995 hadi tani milioni 9.79 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 27.14. Takwimu za Uwiano wa Kujitosheleza kwa Chakula *(Food Self Sufficiency Ratio - SSR)* kuanzia mwaka wa 1994 hadi mwaka wa 2004 zinaonyesha kwamba Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 100.55 **(Kiambatisho Na. 1).**

**Hali ya Chakula kwa Mwaka wa 2004/2005**

**15. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2003/2004 uzalishaji wa mazao ya chakula ulifikia tani milioni tisa, zikiwemo tani milioni 4.93 za nafaka na tani milioni 4.07 za mazao mengine. Mahitaji ya chakula kwa mwaka wa 2004/2005 yalikuwa tani milioni 8.61. Taifa lilijitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya tani milioni 0.39 kabla ya kuongeza albaki ya msimu wa 2002/2003 ambayo ilikuwa tani 209,405. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa hali ya chakula kwa ujumla ilikuwa nzuri, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Shinyanga, Dodoma, Kilimanjaro, Lindi, Mwanza, Mtwara, Arusha, Manyara, Singida, Mara, Iringa na Pwani. Serikali imeagiza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikae na Wilaya zinazopata upungufu wa chakula wa mara kwa mara na kubaini sababu za kuendelea kuwepo kwa tatizo hilo na kubuni mbinu endelevu za kuondokana nalo.

**Matarajio ya Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka wa 2005/2006**

**16. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka wa 2004/2005 iliyofanywa mwezi wa Mei, 2005, inaonyesha kwamba uzalishaji wa chakula utafikia tani milioni 9.79 wakati mahitaji ya chakula kwa mwaka wa 2005/2006 yatakuwa tani milioni 9.55.

Hivyo, inatarajiwa kuwa Taifa litajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 103. Aidha, tathmini hiyo inaonyesha kwamba Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Iringa, Morogoro, Mtwara, Kigoma, Kagera, Pwani na Tanga itakuwa na ziada ya chakula. Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Dodoma, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Singida, Mara, Tabora na Lindi itakuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula kwa viwango na sababu tofauti. Upungufu wa chakula kwa mikoa ya Shinyanga, Dodoma, Singida, Tabora na Wilaya za Hanang na Babati za mkoa wa Manyara, unatokana na kuwepo kwa kipindi kirefu cha ukame kati ya miezi ya Januari na Februari, 2005. Ukame huo ulisababisha kunyauka kwa takriban asilimia 70 ya zao la mahindi. Hata hivyo, sehemu kubwa ya mazao ya mtama na muhogo katika Mikoa hiyo haikuathiriwa sana na ukame. Upungufu wa chakula kwa mikoa ya Mwanza na Mara unatokana na kuchelewa kwa mvua za masika. Kwa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro upungufu wa chakula unatokana na uhaba na mtawanyiko mbaya wa mvua za masika. Tathmini ya kina ya kubaini kaya zitakazoathirika zaidi na upungufu wa chakula itafanyika miezi ya Julai na Agosti, 2005. Tatizo la upungufu wa chakula katika maeneo mengi ya nchi, linatokana na wananchi kutokuzingatia maelekezo wanayopewa ya kulima mazao yanayostahimili mazingira ya maeneo yao.

**Hali ya Chakula katika nchi za Afrika Mashariki na Kati**

**17. Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ya mwezi wa Aprili, 2005 kuhusu matarajio ya chakula katika mwaka wa 2005/2006, inaonyesha kwamba nchi ya Kenya itakuwa na mvua za kutosha hata hivyo kutakuwa pungufu wa chakula katika Jimbo la Mashariki na Wilaya za Mwambao. Nchi ya Uganda itakuwa na hali nzuri ya chakula isipokuwa maeneo ya Kaskazini mwa nchi hiyo ambako vita

vimeathiri uzalishaji wa mazao ya chakula. Nchi ya Eritrea itakuwa na upungufu wa chakula kwa watu takriban milioni 2.3 na katika nchi ya Ethiopia wa milioni 3.133. Nchi za Somalia, Jamhuri ya Kongo na Rwanda zitakuwa na upungufu wa chakula kutokana na kuchelewa kuanza au kutopatikana kwa mvua za kutosha. Nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo zitakuwa na upungufu wa chakula kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

**Hali ya Chakula katika Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)**

**18. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya mwezi wa Mei, 2005 inaonyesha kwamba nchi nane za kusini mwa Afrika zitakuwa na upungufu wa chakula. Namibia itakuwa na upungufu wa tani 136,000, Botswana, tani 292,000, Lesotho, tani 257,000, Malawi, tani 964,000, Msumbiji, tani 31,000, Swaziland, tani 68,000, Zambia, tani 114,000 na Zimbabwe, tani 2,440,000. Upungufu huo wa chakula unatokana na kuchelewa kuanza au kutopatikana kwa mvua za kutosha. Afrika ya Kusini itakuwa na ziada ya tani milioni 5.14 na Angola itajitosheleza kwa chakula, isipokuwa kwa majimbo ya Cunene, Namibe na Kwanza yaliyokumbwa na mafuriko.

**Uzalishaji wa Mazao ya Biashara**

**19. Mheshimiwa Spika**, kati ya mwaka wa 1994/1995 na 2004/2005 uzalishaji wa mazao makuu ya biashara uliongezeka. Zao la chai liliongezeka kwa asilimia 25.49, kahawa, asilimia 27.06; katani, asilimia 7.11; korosho, asilimia 28.7; pamba, asilimia 181. 45; pareto, 108.333; sukari, asilimia 119.48 na tumbaku asilimia 81.71, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.

1. Maelezo ya uzalishaji kwa mazao hayo ni kama ifuatavyo:

**Chai**

**20. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa zao la chai uliongezeka kutoka tani 25,500 zilizozalishwa mwaka wa 1994/1995 hadi tani 32,000 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 25.5. Ongezeko hilo lilitokana na kupatikana kwa soko la uhakika la majani mabichi ya chai katika viwanda vya Katumba, Lupembe, Maruku na Mponde baada ya ubinafsishaji wa viwanda hivyo. Aidha, wakulima wamefufua mashamba yaliyokuwa yametelekezwa na kuongeza matumizi ya mbolea. Uzalishaji wa chai wa wakulima wadogo uliongezeka kutoka tani 4,922 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 8,676, mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 76.3. Chai iliyouzwa nje ya nchi iliongezeka kutoka tani 19,694 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 24,372 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 23.8. Katika kipindi hicho, Taifa lilijipatia jumla ya shilingi 32,629,211,000 kutokana na mauzo ya chai. Kati ya hizo, shilingi 10,845,809,170 zilitokana na soko la ndani na shilingi 32,629,211,000 zilitokana na mauzo ya chai katika soko la nje.

**Kahawa**

**21. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa kahawa uliongezeka kutoka tani 42,500 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 54,000 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 27.1. Ongezeko hilo la uzalishaji limetokana na upandaji wa miche bora yenye ukinzani dhidi ya magonjwa ya chulebuni *(coffee berry disease - CBD)* na kutu ya majani, kupanuliwa kwa maeneo yanayozalisha kahawa, hususan katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kufufuliwa kwa mashamba makubwa ya kahawa katika mikoa ya Kaskazini. Sababu nyingine ni upatikanaji wa soko la uhakika kwa kahawa yenye ubora wa juu na bei

nzuri ya wastani wa Dola za Kimarekani 2.5 kwa kilo, ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 1.7 kwa kilo. Kutokana na hali hiyo, vikundi vya wakulima vinavyouza kahawa yenye ubora wa juu vimeongezeka kutoka vikundi 265 mwaka wa 2000 hadi 318 mwaka wa 2005.

**22. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa shilingi milioni 700 kwa Halmashauri za Wilaya za Kigoma Vijijini, Bukoba Vijijini, Tarime, Arumeru, Mwanga, Moshi Vijijini, Hai, Rombo, Lushoto, Mbeya Vijijini, Rungwe, Ileje, Mbozi na Mbinga kwa ajili ya kununua na kukarabati viwanda vya kati vya kupukuchulia kahawa kama sehemu ya mchango wake katika kuwasaidia wakulima wa kahawa kuongeza ubora wa kahawa wanayozalisha. Uuzaji wa kahawa nje ya nchi uliongezeka kutoka tani 31,990 zilizokuwa na thamani ya shilingi bilioni 32.83 mwaka wa 2003/2004 hadi tani 51,793 zilizokuwa na thamani ya shilingi bilioni 65.44 mwaka wa 2004/2005.

**Katani**

**23. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa katani uliongezeka kutoka tani 25,022 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 26,800 mwaka wa 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 7.1. Ongezeko hilo limetokana na kufufuliwa kwa mashamba ya mkonge baada ya ubinafsishaji na ushirikishwaji wa wakulima wadogo kilimo cha mkonge. Katika mwaka wa 2003/2004, jumla ya wakulima wadogo 2,415 walizalisha tani 3,269 za katani. Katika mwaka wa 2004/2005, mapato yaliyotokana na mauzo ya katani nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 8.214 kutokana na mauzo ya tani 11,675.57 za katani.

**Korosho**

**24. Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa korosho uliongezeka kutoka tani 63,400 mwaka wa 1994/1995, hadi tani 81,600 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 28.7. Katika mwaka wa 2000/2001 uzalishaji wa korosho ulifikia tani 122.30. Ongezeko hilo lilitokana na wakulima kupata bei nzuri, ufufuaji wa mashamba ya mikorosho na upandaji wa mbegu bora iliyozalishwa na Kituo cha Utafiti cha Naliendele, Mtwara. Aidha, jumla ya viwanda 11 vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali vimebinafsishwa na ukarabati wa viwanda hivyo unaendelea ili usindikaji wa korosho uanze katika mwaka wa 2005/2006. Katika mwaka wa 2004/2005, tani 66,983 ziliuzwa nje na kuliingizia Taifa mapato ya shilingi bilioni 61.53.

**Pamba**

**25. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa zao la pamba uliongezeka kutoka tani 122,300 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 344,207 mwaka wa 2003/2004, sawa na ongezeko la asilimia 181.4. Ongezeko hilo limevuka kiwango cha juu kilichowahi kuzalishwa mwaka wa 1992/1993 cha tani 287.5. Mafanikio hayo yalitokana na bei nzuri za pamba katika msimu uliotangulia, kupanuliwa kwa maeneo yaliyolimwa pamba, kuongezeka kwa matumizi ya viuatilifu, mbegu bora, mbolea na pia yalitokana na mvua zilizonyesha kwa mtawanyiko mzuri. Katika msimu wa 2004/2005, mapato yaliyotokana na mauzo ya pamba nyuzi nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 44.38.

**Pareto**

**26. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa pareto uliongezeka kutoka tani 480 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 1,000 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 108. Katika mwaka wa 2001/2002 uzalishaji wa pareto ulipanda hadi tani 3,500 na kushuka hadi kufikia tani 1,000 mwaka wa

2004/2005. Kushuka kwa uzalishaji wa pareto kumechangiwa na kukosekana kwa soko la uhakika la zao hilo.

**Sukari**

**27. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa sukari uliongezeka kutoka tani 104,620 zilizozalishwa mwaka wa 1994/1995 hadi tani 229,617 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 119.5. Ongezeko hilo limechangiwa na kukarabatiwa na kufufuliwa kwa mashamba ya miwa na viwanda vya sukari vya Kilombero I na II, Mtibwa, TPC na Kagera baada ya ubinafsishaji. Aidha, ushirikishwaji wa wakulima wadogo (*Cane Outgrowers*) chini ya utaratibu wa kilimo cha mkataba katika viwanda vya Kilombero na Mtibwa umechangia kupanua eneo linalozalisha miwa. Wakulima wadogo wa miwa wameongezeka kutoka 4,000 mwaka wa 1994/1995 hadi 9,000 mwaka wa 2004/2005. Katika kipindi hicho, sukari iliyouzwa nje ya nchi iliongezeka kutoka tani 10,700 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 22,278 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 108.2. Katika msimu wa 2004/2005, mapato yaliyotokana na mauzo ya sukari nje ya nchi yalikuwa shilingi bilioni 12.21. Aidha, sukari iliyozalishwa na kuuzwa hapa nchini mwaka wa 2004/2005 ilikuwa tani 207,339 yenye thamani ya shilingi bilioni 111.55, ikilinganishwa na tani 94,121 zenye thamani ya shilingi bilioni 33.88 za mwaka wa 1994/1995.

**Tumbaku**

**28. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa tumbaku uliongezeka kutoka tani 28,600 mwaka wa 1994/1995 hadi tani 51,972 mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 81.7. Ongezeko hilo lilitokana na matumizi ya mbegu bora aina za K326, UIT10 na RG17, mbolea ya NPK 10:18:24, kuimarishwa

kwa huduma za ugani na upatikanaji wa soko la uhakika. Mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima iliyotolewa na wanunuzi wa tumbaku ilichangia kuwaongezea wakulima uwezo wa kumudu gharama za pembejeo. Kutokana na juhudi hizo, tija katika uzalishaji wa tumbaku iliongezeka kutoka kilo 782 kwa hekta mwaka wa 1994/1995 hadi kilo 920 kwa hekta mwaka wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 17.7. Aidha, ubora wa tumbaku uliongezeka kwa asilimia 15, kwa madaraja ya juu na kupungua kwa asilimia 10 kwa madaraja ya chini. Uuzaji wa tumbaku nje ya nchi uliongezeka kutoka tani 17,019 zilizokuwa na thamani ya shilingi bilioni 16.633 katika mwaka wa 1994/1995 hadi tani 34,861 zilizokuwa na thamani ya shilingi bilioni 81.990 katika mwaka wa 2004/2005.

***Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara kuanzia Mwaka wa 1994/95 hadi 2004/2005 (TANI '000)***

| Mwaka | Pamba | Kahawa | Korosho | Pareto | Sukari | Tumbaku | Chai | Mkonge |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1994/1995 | 122.30 | 42.50 | 63.40 | 0.48 | 104.62 | 28.60 | 25.50 | 25.02 |
| 1995/1996 | 250.20 | 53.30 | 81.73 | 0.44 | 116.81 | 35.41 | 21.16 | 23.62 |
| 1996/1997 | 252.90 | 44.30 | 63.03 | 0.26 | 116.10 | 51.23 | 19.94 | 22.00 |
| 1997/1998 | 203.20 | 38.00 | 99.92 | 0.43 | 116.10 | 37.98 | 26.47 | 20.00 |
| 1998/1999 | 105.40 | 42.70 | 106.44 | 0.50 | 113.62 | 26.49 | 21.88 | 23.23 |
| 1999/2000 | 192.70 | 48.80 | 121.21 | 1.00 | 116.93 | 24.83 | 24.13 | 20.90 |
| 2000/2001 | 123.56 | 58.10 | 122.30 | 1.90 | 135.53 | 27.70 | 26.39 | 20,,5 |
| 2001/2002 | 148.18 | 36.20 | 67.40 | 3.50 | 163.99 | 27.89 | 24.73 | 23.54 |
| 2002/2003 | 188.89 | 52.40 | 95.00 | 3.00 | 190.10 | 33.55 | 28.03 | 23.64 |
| 2003/2004 | 137.90 | 37.50 | 80.00 | 2.00 | 228.00 | 47.73 | 30.70 | 23.86 |
| 2004/2005 | 344.21 | 54.00 | 81.60 | 1.00 | 229.62 | 51.97 | 32.00 | 26.80 |
| JUMLA | 2,069.44 | 507.80 | 982.03 | 14.51 | 1,631.42 | 393.38 | 280.93 | 232.61 |
| Asilimia* | 181.45 | 27.06 | 28.71 | 108.33 | 119.48 | 81.71 | 25.49 | 7.11 |

* Asilimia ya ongezeko kutoka mwaka 1994/1995 hadi 2004/2005.

Chanzo: Bodi za mazao 2005

## Mazao ya Mboga, Matunda na Maua

**29. Mheshimiwa Spika,** kuyumba kwa bei za mazao makuu ya biashara katika soko la dunia, hususan kuanzia miaka miaka ya 1980, kumelilazimu Taifa kutafuta mazao mengine ambayo yana bei nzuri na uhakika wa upatikanaji wa masoko. Hali hiyo imesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mboga, matunda, viungo na maua. Wizara imeendelea kufanya utafiti ili kupata aina bora za mbegu za mboga matunda na viungo kwa lengo la kuzisambaza kwa wakulima. Matokeo ya juhudi hizo, yameanza kuonekana kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao hayo. Kwa mfano, mwaka wa 2003/2004 uzalishaji wa mazao ya mboga ulikadiriwa kufikia tani 603,000 ikilinganishwa na tani 542,700 zilizozalishwa katika mwaka wa 2002/2003.

**30.** Katika msimu wa 2004/2005, Wizara iliendelea kusambaza miche bora ya mazao ya mboga, matunda, migomba na viungo kwa wakulima katika meneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi wa Mei, 2005, jumla ya vipando 200,000 vya migomba vilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Jumla ya miche 108,255 ya miti ya matunda, minazi na viungo ilizalishwa katika bustani zinazosimamiwa na Wizara na kusambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Pwani, Kigoma, Tanga, Mbeya, Morogoro na Dar es Salaam. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya tani 6,868 za maua zilizalishwa; kati ya hizo, tani 4,479.79 za maua ziliuzwa nje na kulipatia Taifa jumla ya shilingi bilioni 15.0.

## SABABU ZILIZOCHANGIA KUONGEZEKA KWA UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO

**31. Mheshimiwa Spika,** kuanzia mwaka wa 1994/1995 hadi mwaka 2004/2005, Serikali imekuwa ikichukua hatua za makusudi zinazolenga

kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuweka utaratibu na mipango ya kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kupanua maeneo ya mashamba kwa kuongeza matumizi ya wanyamakazi na matrekta, kupanua maeneo yanayozalisha kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kuongeza kiasi cha bajeti ya Serikali kinachotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo.

**Upatikanaji wa Pembejeo na Zana za Kilimo**

**32. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2000/2001, Wizara ilifanya tathmini ya mifumo ya upatikanaji wa pembejeo na zana bora za kilimo ili kubaini mfumo utakaohakikisha pembejeo zinapatikana kwa wingi na kwa ubora unaotakiwa katika mazingira ya soko huru. Aidha, Wizara imeimarisha uwezo wa taasisi zinazosimamia huduma za pembejeo, Wakala wa Mbegu wa Taifa, Taasisi ya Kusimamia Ubora wa Mbegu, Vituo vya Utafiti wa Kilimo na Ofisi ya Msajili wa mbegu na Mimea mipya.

**Mfuko wa Taifa wa Pembejeo**

**33. Mheshimiwa Spika,** rasilimali za Mfuko wa Taifa wa Pembejeo zimekuwa zikiongezwa ili kuwahudumia wateja wengi zaidi. Kati ya mwaka wa 2000/2001 na mwaka wa 2004/2005, jumla ya shilingi 8,902,145,800 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya mikopo ya pembejeo na zana. Kati ya hizo, shilingi 456,730,000 zilitolewa mwaka wa 2001/2002, shilingi 2,500,000,000 zilitolewa mwaka wa 2002/2003, shilingi 2,628,082,300 zilitolewa mwaka wa 2003/2004 na shilingi 3,107,333,500 zilitolewa mwaka wa 2004/2005. Katika kipindi hicho, jumla ya shilingi 9,773,452,878 zilitolewa kama mikopo

kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo, matrekta mapya na kugharamia ukarabati wa matrekta mabovu. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza uanzishwaji wa Mifuko ya Maendeleo ya Mazao makuu ya biashara. Kwa mfano, Mfuko wa Kuendeleza zao la Pamba umekuwa na manufaa makubwa katika zao la pamba na hivi sasa unagharamia zaidi ya asilimia 80 ya pembejeo zinazotumika katika uzalishaji wa pamba.

**Ruzuku kwa Pembejeo za Kilimo**

**34. Mheshimiwa Spika,** kuanzia mwaka wa 2003/2004, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa ruzuku ya kugharamia usafirishaji na sehemu ya bei ya baadhi ya mbolea. Katika mwaka wa 2003/2004, shilingi bilioni 2.0 zilitumika kufidia gharama za usafirishaji wa jumla ya tani 39,387 za mbolea kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Katika mwaka wa 2004/2005, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 7.244 kwa ajili ya kugharamia utaratibu huo kwa mikoa yote ya Tanzania Bara. Hadi mwezi wa Juni 2005, jumla ya tani 81,766 za mbolea zilisafirishwa na kuuzwa chini ya utaratibu huu. Aidha, kuanzia mwezi wa Mei, 2005, Serikali imeanza kutoa ruzuku kwa ajili ya madawa ya mikorosho na matengenezo ya mabomba ya kunyunyuzia madawa hayo. Chini ya utaratibu huo, Serikali italipia gharama za usafirishaji wa madawa ya ubwiri unga yenye madhara madogo kwa mazingira kwa asilimia 100 na itatoa ruzuku ya kulipia nusu ya bei za madawa hayo na pia kugharamia matengenezo na marekebisho ya mabomba ya kupulizia dawa ili yaweze kutumiwa kwa dawa za maji.

**35.** Mafanikio ya utekelezaji wa utaratibu wa ruzuku yameanza kuonekana katika kuongezeka kwa matumizi ya mbolea. Mwaka wa 2003/2004 tani 125,653.0 za mbolea zilitumika. Kiasi hicho kiliongezeka na kufikia tani

195,065.0 zilizotumika katika msimu wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 55.2. Aidha, ongezeko la matumizi ya mbolea limechangia katika kasi ya kukua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Katika mwaka wa 2004, sekta ndogo ya mazao ya kilimo ilikua kwa asilimia 6.2.

**36. Mheshimiwa Spika,** ili kupanua maeneo yanayolimwa na kuwapunguzia wakulima harubu zitokanazo na matumizi ya zana duni katika uzalishaji, Wizara imeendelea kuhimiza kilimo cha matrekta, wanyamakazi na matumizi ya mikokoteni. Kati ya mwaka wa 2000/2001 na 2004/2005, jumla ya matrekta makubwa 1,598, matrekta madogo zaidi ya 569 na plau 197,522 ziliingizwa nchini. Ili kuwaongezea wakulima uwezo wa kutumia zana zinazokokotwa na wanyamakazi, Wizara ilikarabati vituo 53 vya kufundishia wanyamakazi. Hadi mwezi wa Juni, 2005, jumla ya wakulima 11,295 na wataalam 1,539 walikuwa wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya zana zinazokokotwa na wanyamakazi. Aidha, wakulima 7,220 na wataalam 225 walipatiwa mafunzo ya matumizi na matunzo ya matrekta madogo ya mikono katika vituo hivyo.

**Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani**

**37. Mheshimiwa Spika,** kati ya mwaka wa 2001 na 2002, Serikali ilifanya tathmini ya kina kubaini maeneo yanayofaa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kuandaa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Mpango huo, umeainisha jumla ya hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani; hekta milioni 2.3 zenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa, hekta milioni 4.8 zenye uwezekano wa wastani wa kuendelezwa na hekta milioni 22.3 zenye uwezekano mdogo wa kuendelezwa. Katika kutekeleza mpango huo, Wizara

ilitoa kipaumbele katika ukarabati wa skimu na mabwawa yaliyojengwa katika miaka iliyopita, ujenzi wa miradi mipya, hususan ile ya gharama nafuu na yenye uwezekano wa kuhudumia watu wengi na ujenzi wa mabwawa ili kuwezesha uvunaji wa maji ya mvua, hususan kwenye maeneo yenye ukame. Aidha, Wizara imejenga miradi ya mfano ya umwagiliaji maji mashambani katika mwambao wa Ziwa Viktoria kwa lengo la kuwahamasisha wananchi ili waige miradi hiyo na kuanzisha ukanda wa kijani kuzunguka Ziwa Viktoria.

**38.** Kati ya mwaka wa 2001/2002 na mwaka wa 2004/2005, jumla ya skimu 105 zenye eneo la hekta 58,092 ziliendelezwa. Katika mwaka wa 2001/2002 hekta 4,806 ziliendelezwa, hekta 11,242 katika mwaka wa 2002/2003, hekta 23,970 mwaka wa 2003/2004 na hekta 22,506 ziliendelezwa katika mwaka wa 2004/2005. Hivyo, eneo lililoendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani limefikia hekta 249,992. Aidha, tija na uzalishaji wa mazao, hususan zao la mpunga katika maeneo ya umwagiliaji maji mashambani, imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 za mpunga kwa hekta hadi wastani wa tani 5.0 kwa hekta.

**Jedwali Na. 2. Maeneo yaliyoendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani tangu mwaka wa 2001/2002 hadi 2004/2005**

| Mwaka | Eneo Lililoendelezwa (Hekta) | Mavuno Ya Mpunga (Tani) |
|---|---|---|
| 2001/2002 | 191,900 | 767,600 |
| 2002/2003 | 200,895 | 803,580 |
| 2003/2004 | 227,486 | 909,944 |
| 2004/2005 | 249,992 | 999,968 |

Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula

## Hifadhi ya Chakula

**39. Mheshimiwa Spika,** Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa Hifadhi ya Chakula ya Taifa ina akiba ya chakula ya kuiwezesha kukabiliana na dharura za upungufu wa chakula. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali ilinunua jumla ya tani 255,600 za chakula zilizotumiwa kukabiliana na upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali ya nchi. Tani 55,300 za mahindi zilinunuliwa mwaka wa 2000/2001, tani 9,800 mwaka wa 2001/2002, tani 27,500 mwaka wa 202/2003, tani 56,000 mwaka wa 2003/2004 na tani 97,842 mwaka wa 2004/2005 (hiki ndicho kiasi kikubwa cha chakula kuwahi kununuliwa katika msimu mmoja). Hadi tarehe 15 Juni, 2005, Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa na jumla ya tani 113,148 za mahindi.

**40.** Aidha, katika mwaka wa 2002/2003 Taifa lilijitosheleza kwa chakula kwa wastani wa asilimia 102. Katika mwaka huo nchi za Malawi, Zambia na Zimbabwe zilikuwa zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula. Serikali ilitoa msaada wa tani 2,000 kwa nchi ya Malawi, tani 2,000 kwa Zambia na tani 3,000 kwa Zimbabwe. Misaada hiyo, imetujengea heshima kubwa kwani kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania huru, Serikali ilitoa msaada wa chakula kwa nchi zilizokabiliwa na upungufu wa chakula.

## Huduma za Ushauri kwa Wakulima

**41. Mheshimiwa Spika,** kuanzia mwaka wa 1998/1999 jumla ya maafisa 7,800 walihamishiwa kwenye Halmashauri za Wilaya, chini ya Mpango wa Kurekebisha Serikali za Mitaa (*Local Government Reform Programme*), ambapo maafisa ugani walikuwa 3,898. Maafisa hao wanasimamiwa na

Serikali zao za Mitaa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**42.** Aidha, kati ya mwaka wa 2000/2001 na 2004/2005, Serikali iliwapandisha vyeo jumla ya watumishi wa kilimo 2,564 ili kuongeza ari katika utendaji wa kazi. Katika kipindi hicho, jumla ya maafisa ugani 1,600 walipatiwa mafunzo ya kuimarisha taaluma zao. Kati ya hao, maofisa ugani watano walipata mafunzo ya ngazi ya Shahada, 200 ya stashahada na 1,395 mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Wizara iliendelea kuwapatia wataalam wa kilimo vifaa mbalimbali vya kutendea kazi yakiwemo, magari 52, pikipiki 100 na baiskeli 1,200.

**Udhibiti wa Wanyama, Ndege na Wadudu Waharibifu wa Mazao**

**43.** **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao, hususan milipuko ya nzige, *Quelea quelea*, viwavijeshi, panya na magonjwa mbalimbali ya mimea, Wizara imeendelea kujenga uwezo wake na wa wakulima wa kupambana na visumbufu hivyo. Kati ya mwaka wa 2000/2001 na 2004/2005 Wizara imeimarisha uwezo wake wa kutambua milipuko na kushirikiana na mashirika ya kimataifa, hususan Mashirika ya kupambana na nzige wekundu na wa jangwani, kudhibiti visumbufu hivyo. Aidha, Wizara iliendelea kutumia mbinu ya udhibiti wa kibaolojia kwa mafanikio makubwa. Kwa mfano, milipuko ya kidung'ata wa mihogo, imedhibitiwa kwa ufanisi mkubwa kwa kuwatumia wadudu maadui. Aidha, udhibiti wa kibaolojia wa gugumaji katika ziwa viktoria kwa kutumia wadudu aina ya mbawakavu ulifanyika kwa mafanikio makubwa.

**44.** Kati ya mwaka wa 2000/2001 na mwaka wa 2004/2005, Wizara ilitumia jumla ya shilingi 4,273,153,312 kugharamia kazi za udhibiti wa visumbufu

vya mimea na mzao.  Kati ya hizo, shilingi 301,844,000 zilitumika mwaka wa 2000/2001, shilingi 462,473,100 mwaka wa 2001/2002, shilingi 613,206,762 mwaka wa 2002/2003, shilingi 945,000,000 mwaka wa 2003/2004 na shilingi 2,252,473,450 mwaka wa 2004/2005.

**Kuongezeka kwa Uwekezaji Katika Kilimo**

**45.** Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa 2002/2003, Serikali imekuwa ikiongeza kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo.  Kwa mfano, katika mwaka wa 2002/2003, Wizara ya Kilimo na Chakula ilipewa jumla ya shilingi 34,328,494,605, shilingi 54,146,806,100 katika mwaka wa 2003/2004 na shilingi 64,074053,600 katika mwaka wa 2004/2005 na katika makisio ya 2005/2006 kiasi cha shilingi, 118,124,823,900 kinaombwa ambacho ni sawa na asilimia 84.4 ikilinganishwa na kiasi kilichotengwa katika mwaka wa 2004/2005.  Nyongeza ya fedha zilizotolewa na Serikali ilielekezwa kwenye mambo ambayo yalitarajiwa kuwa na mafanikio katika muda mfupi na ambayo yalikuwa na manufaa ya moja kwa moja kwa mkulima.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI, MAFANIKIO NA MATUMIZI YA FEDHA ZILIZOIDHINISHWA NA KUTOLEWA KATIKA MWAKA WA 2004/2005

**46.** **Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2004/2005, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 64.074. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 34.976 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 29.097 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 6.436 zilikuwa za ndani na shilingi bilioni 22.661 zilikuwa za nje.

**Matumizi ya Kawaida**

**47. Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Juni, 2005, Wizara ilipokea kutoka Hazina jumla ya shilingi 34,697,177,375.17 sawa na asilimia 98.05 ya kiasi kilichoidhinishwa. Hadi tarehe 15 Juni, 2005, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi 34,265,405,375.06 sawa na asilimia 98.80 ya kiasi kilichotolewa.

**Matumizi ya Miradi ya Maendeleo**

**48. Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 15 Juni, 2005 shilingi 6,436,433,200 fedha za ndani zilikuwa zimetumika, sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, shilingi 13,744,665,601.85 fedha za nje sawa na asilimia 80.6 ya fedha zilizotolewa (shilingi 17,062,210,292) zilikuwa zimetumika kugharamia shughuli za miradi. Matumizi haya ni sawa na asilimia 70 ya fedha za nje zilizotolewa. Matumizi haya madogo yanatokana na muda mrefu unaotumika kukamilisha taratibu za zabuni za vifaa na huduma. Uwezo mdogo wa kuibua na kutekeleza miradi katika wilaya zinazotekeleza mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (PADEP) umechangia katika matumizi madogo. Baadhi ya wafadhili wameshindwa kutimiza ahadi zao. Kwa mfano, Benki ya Dunia iliahidi kutoa jumla ya shilingi milioni 905.8 kwa ajili ya maandalizi na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Huduma za Kilimo (*Agricultural Service Support Programme-ASSP*), fedha hizo hazikutolewa kwa sababu hawakuwa wamezitenga. Aidha, Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU) hawakutoa fedha za STABEX shilingi bilioni 4.7 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) kama walivyokuwa wameahidi.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO *(ASDP)*

**49. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2004/2005, ulikuwa mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Wizara za Sekta ya Kilimo ambazo zinajumuisha Wizara za Ushirika na Masoko, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Kilimo na Chakula na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, zimeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu hiyo.

### Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPS)

**50. Mheshimiwa Spika,** sehemu kubwa ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo inatekelezwa katika wilaya na vijiji kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans - DADPs).* Katika mwaka wa 2004/2005, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Fedha hizo zinatumika katika kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wakulima kwa njia shirikishi kama sehemu ya mipango ya maendeleo ya wilaya. Miradi iliyoibuliwa ambayo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali ni pamoja na uchimbaji wa malambo, ujenzi wa majosho, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani, uimarishaji wa vyama vya kuweka na kukopa, kilimo cha wanyamakazi, uboreshaji wa kuku na mbuzi wa kienyeji, uendelezaji wa ng'ombe wa maziwa, uendelezaji wa mazao, hifadhi ya udongo, udhibiti wa visumbufu vya mazao, ujenzi wa minada, ununuzi wa mashine za kupukuchua na kusafisha kahawa, usindikaji wa mazao na uzalishaji wa mbegu. Ili kuhakikisha kazi zilizopangwa chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya zinatekelezwa, Wilaya zinasimamia utekelezaji wa miradi iliyoidhinishwa kutekelezwa, zinafuatilia na kuandaa

taarifa za utekelezaji na kuwasilisha mikoani na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara za Sekta ya Kilimo.

**Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*PADEP*)**

**51. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005 Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji umeendelea kutekelezwa katika wilaya 29 za Tanzania Bara na wilaya tano za Zanzibar. Wilaya za Tanzania Bara ni Arumeru, Hai, Iringa, Morogoro, Singida, Hanang, Monduli, Masasi, Nachingwea, Mbulu, Karatu, Iramba na Kiteto. Nyingine ni Sikonge, Uyui, Urambo, Babati, Moshi, Rombo, Same, Mwanga, Ulanga, Kilombero, Handeni, Kilindi, Korogwe, Lushoto, Kilolo na Mvomero. Wilaya za Zanzibar ni Magharibi, Kaskazini A na Kati zilizoko Unguja na Chake Chake na Wete zilizoko Pemba. Lengo kuu la PADEP ni kuchangia katika juhudi za kutokomeza umaskini kwa kuongeza tija katika sekta ya kilimo. Ili kufikia lengo hilo Mradi unatekeleza mikakati ifuatayo:

***(i) Kujenga Uwezo wa Wakulima na Wafugaji kwa kutumia Teknolojia Mpya na Sahihi na kwa Kuwashirikisha katika kufanya Maamuzi, Kupanga, Kutekeleza na Kusimamia Mipango ya Maendeleo yao***

**52. Katika mwaka wa 2004/2005, vikundi 810 vya wakulima na wafugaji kutoka kaya 33,506 viliundwa. Wakulima katika vikundi hivyo waliibua na kutekeleza miradi mbalimbali 1,001 baada ya kupatiwa mafunzo. Mafunzo mengine yalihusu ufuatiliaji na tathmini shirikishi, utunzaji na usimamizi shirikishi wa fedha, ununuzi wa bidhaa na huduma, ushiriki wa sekta binafsi na utunzaji na hifadhi ya mazingira. Aidha, wilaya zinazotekeleza mradi zilipewa vitendea kazi, ambavyo ni**

**pamoja na magari 16 na kompyuta 16. Jumla ya shilingi bilioni 3.3 zilitumika katika maandalizi na utekelezaji wa miradi hiyo.**

***(ii) Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi katika shughuli za Uzalishaji, Utoaji Huduma na Masoko ili kuongeza Tija na Mapato ya Wakulima na Wafugaji***

**53.** **Mheshimiwa Spika**, hadi mwishoni mwa mwaka wa 2004/2005, vijiji 192 vilikuwa vinatekeleza miradi ipatayo 949 iliyogharimu jumla ya shilingi bilioni 8.8. Miradi hiyo ya wakulima na wafugaji iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ambapo miradi mikubwa tisa ya vijiji na 494 ya vikundi vya wakulima na wafugaji imekamilika. Miradi iliyokamilika inahusu ujenzi wa mabanio na mifereji ya umwagiliaji maji mashambani katika vijiji vya Mungushi na Kware, Hai na kijiji cha Dihombo, Mvomero. Aidha, vijiji vya Itaja, Mangida, Muhitiri na Mipilo, Singida pamoja na Gehandu na Dirma, Hanang tayari vimekamilisha miradi sita ya uchimbaji wa malambo na ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo. Miradi mingine iliyopo katika hatua za mwisho ni ujenzi wa maghala ya mazao katika vijiji vya Mandawa, Reje, Ndomondo na Mtimbo wilayani Nachingwea pamoja na vijiji vya Chikundi, Maratani, Maugura, Namajani na Msikisi wilayani Masasi. Miradi 446 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo ni uboreshaji mifugo (asilimia 28.5), uendelezaji mazao na kutumia mbegu bora na pembejeo (asilimia 15.9), matumizi ya zana bora za kilimo (asilimia 11). Miradi mingine inahusu usindikaji wa mazao (asilimia 3), uboreshaji wa miundombinu ya masoko (asilimia 4.7) na hifadhi ya mazingira (asilimia 12.3). (**Kiambatisho 2**).

**54.** Shughuli za kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uzalishaji, utoaji huduma na masoko zilitekelezwa kwa kuwashirikisha wakulima na wafugaji

katika kupanga, kutekeleza na kuchangia gharama za utekelezaji. Hadi tarehe 31 Mei, 2005, wakulima wamechangia takriban shilingi milioni 601.4 ambazo ni karibu asilimia 30 ya fedha zote zilizotolewa na PADEP katika utekelezaji wa miradi hiyo. Ushiriki huo unadhihirisha kuwa wakulima wako tayari kumiliki na kuchangia maendeleo ya miradi yao wenyewe.

***(iii) Kuimarisha Uwezo wa Halmashauri za Wilaya na Taasisi husika za Serikali Kuu na Sekta Binafsi katika ngazi za Kijiji, Wilaya na Taifa katika huduma kwa Wakulima na Wafugaji***

**55. Mheshimiwa Spika**, wilaya 8 za Hai, Arumeru, Morogoro, Iringa, Masasi, Nachingwea, Singida na Hanang zimeunda kamati za kuratibu ushiriki wa sekta binafsi katika kuimarisha kilimo. Kamati hizo zina wajibu wa kubainisha vikwazo na fursa zilizopo na namna ya kuimarisha usambazaji na uuzaji wa pembejeo na mazao ya wakulima. Mradi unaendelea kuhamasisha wilaya 21 zilizobaki ili nazo zianzishe kamati hizo

## KILIMO CHA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI

**Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005 ulikuwa ni mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*National Irrigation Master Plan)* ambapo jumla ya hekta 22,506 ziliendelezwa. Kiasi hiki kinafanya eneo lililoendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani nchini kufikia jumla ya hekta 249,992. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 83 ya lengo la kuendeleza hekta 27,124. Eneo lililoongezeka linajumuisha ujenzi na ukarabati wa skimu 83 za umwagiliaji maji mashambani, ujenzi wa mabwawa 12 na skimu 12 za uvunaji wa maji ya mvua. Aidha, Wizara imejenga skimu 10 za mfano ya umwagiliaji maji mashambani katika mwambao wa ziwa Viktoria kwa lengo la

kuwahamasisha wananchi kuanzisha ukanda wa kijani wa mazao kuzunguka Ziwa Viktoria. Jumla ya shilingi 8,228,179,020 zilitumika katika kuendeleza skimu na mabwawa ya umwagiliaji maji mashambani. Kati ya hizo shilingi 3,266,348,068 ni za hapa nchini na shilingi 4,961,830,951 ni za nje **(Kiambatisho Na. 3).**

**Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani na Ujenzi wa Mabwawa**

**56. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005 skimu 17 zenye jumla ya hekta 5,100 zilikarabatiwa na skimu 4 zenye jumla ya hekta 2,716 zilipimwa na kufanyiwa usanifu. Skimu zilizokarabatiwa ni Nkenge, Bukoba (hekta 40); Ruhwiti, Kibondo (hekta 200); Mahurunga, Mtwara (hekta 500); Nkonkwa, Kigoma Vijijini (hekta 100); Kimwangamao, Moshi Vijijini (hekta 1,200); Ngage, Simanjiro (hekta 650); Misozwe, Muheza (hekta 100); Madizini, Kilosa (hekta 100); Sonjo, Kilombero (hekta 100); Kitaya, Mtwara (hekta 300); Kitanda, Namtumbo (hekta 100); Namatuhi, Songea (hekta 100); Muze/Sakalilo, Sumbawanga (hekta 400); Mang'onyi, Singida (hekta 200); Magubike, Iringa Vijijini (hekta 160); na Mbebe, Ileje (hekta 400). Jumla ya shilingi 789,416,000 zilitumika. Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, wakati wa kuandaa mpango kabambe wa umwagiliaji maji mashambani, skimu 10 za umwagiliaji zilibainishwa gharama zake za ujenzi, uendeshaji wa matengenezo. Skimu hizo ni Kinyope, Lindi (hekta 200), Magoma, Korogwe (hekta 200), Pawaga, Iringa Vijijini (hekta 2,000), Mgongola, Morogoro Vijijini (hekta 680), Lower Moshi, Moshi Vijijini (hekta 1,560), Pamila, Kigoma Vijijini (hekta 30), Nkenge, Bukoba (hekta 50), Luchili, Sengerema (hekta 500), Kisese, Mkuranga (hekta 200) na Musa Mwinjanga, Hai (hekta 646).

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASPS II)***

**57. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2004/2005 ujenzi wa skimu tatu zenye jumla ya hekta 1,970 ulikamilika. Skimu hizo ni Nyanzwa (hekta 760) na Irindi (hekta 610), Kilolo; na Utengule Usongwe, Mbeya Vijijini (hekta 600). Aidha, Ujenzi wa Skimu ya Naming'ongo, Mbozi (hekta 1,000) umefikia asilimia 70 na unatarajiwa kukamilika mwezi wa Deseaba, 2005. Jumla ya shilingi 844,830,951 zilitumika kati ya shilingi 1,878,280,286 zilizotolewa.

**Skimu zilizogharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula (*Food Aid Counterpart Fund*)**

**58.** Katika mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendeleza skimu kumi zenye jumla ya hekta 2,581 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula (*Food Aid Counterpart Fund*). Skimu hizo ni Kikafu Chini, Hai (hekta 641); Mvumi, Kilosa (hekta 293); Mlali, Morogoro Vijijini (hekta 80); Cherehani Mkoga, Iringa Vijijini (hekta 180); Shamwengo, Mbeya Vijijini (hekta 230); Manolo, Nzega (hekta 200); Mkula, Kilombero (hekta 250); Ruaha Mbuyuni, Kilolo (hekta 300), Ipwasi/Ndorobo, Iringa Vijijini (hekta 250) na Nganjoni, Moshi Vijijini (hekta 220). Jumla ya shilingi 604,562,000 zilitumika kwa kazi hiyo.

**Skimu za Mfano za Umwagiliaji Maji Mashambani katika Mwambao wa Ziwa Viktoria**

**59. Mheshimiwa Spika,** Skimu kumi za mfano zenye jumla ya hekta 415 ziliendelezwa kwa kutumia teknolojia za kuvuta maji kwa pampu zinazoendeshwa kwa nguvu ya upepo, mafuta ya dizeli na mionzi ya jua na

pampu za miguu. Aidha, mashamba mengine yanaendelea kupimwa ili teknolojia hiyo itumke pia katika maeneo hayo. Mashamba ya mfano yaliyoendelezwa ni Nyangwi, Nyamagana (hekta 50), Nyashimba A, Ilemela (hekta 40), Sangabuye, Ilemela (hekta 55), Nyang'holongo, Ilemela (hekta 60), Simiyu, Magu (hekta 40), Mwamanyili, Magu (hekta 40), Ilungu, Magu (hekta 20), Lukungu, Magu (hekta 20), Chabula, Magu (hekta 30) na Balili, Bunda (hekta 60). Madhumuni ya skimu hizo ni kuwahamasisha wakulima ili waige kuanzisha skimu kama hizo kwa lengo la kuanzisha ukanda wa kijani wa mazao katika mwambao wa Ziwa Viktoria. Jumla ya shilingi 60,000,000 zilitumika kwa kazi hiyo.

**60.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, skimu nyingine ambazo Serikali iligharamia ukarabati ni pamoja na ujenzi wa mabwawa matano ya Ikowa, Dodoma vijijini (hekta 150), Ruvu NAFCO, Kibaha (hekta 100), Mwangeza, Iramba (hekta 152); Maneke, Musoma (hekta 200) na Kiseriani, Monduli (hekta 30). Aidha, mabwawa saba ya Mkomazi, Korogwe (hekta 200), Tyeme Masagi, Iramba (hekta 200), Kironda Datali, Iramba (hekta 100), Usoke, Urambo (hekta 100) na Nyaishozi, Karagwe (hekta 50), Mwele, Muheza (hekta 100) na Choma cha Nkola, Igunga (hekta 100) yamefanyiwa usanifu. Jumla ya shilingi 740,000,000 zilitumika.

### Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*Participatory Irrigation Development Programme – PIDP*)

**61.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani, imekamilisha ujenzi wa skimu 12 zenye jumla ya hekta 2,465 kwa kujenga majaruba na miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani. Skimu hizo ni Gichameda, Babati (hekta 154),

Qash, Babati (hekta 206); Uhelela, Dodoma (hekta 134), Mpwayungu, Dodoma (hekta 140); Udimaa, Manyoni (hekta 200); Diyomat, Mbulu (hekta 373), Harsha, Mbulu (hekta 250); Tumati, Mbulu, (hekta 112); Sigili, Nzega (hekta 315); Chamipilu, Nzega (hekta 329); Lakuyi, Nzega (hekta 92); na Luhala, Kwimba (hekta 160). Aidha, skimu 12 zenye jumla ya hekta 2,527 ziko kwenye hatua mbalimbali za ujenzi na zinatarajiwa kukamilika kabla ya msimu ujao wa kilimo. Skimu hizo ni Nyida, Shinyanga (hekta 289); Itilima, Shinyanga (hekta 225); Masengwa, Shinyanga (hekta 337); Nyambeho, Misungwi (hekta 180); Msagali, Mpwapwa (hekta 210); Mwangeza, Iramba (hekta 152), Kimiza Kwimba (hekta 153); Shilanona, Kwimba (hekta 201); Mtitaa, Dodoma (hekta 106); Bukigi, Maswa (hekta 150); Igurubi, Igunga (hekta 334); na Mangisa, Mbulu (hekta 190). Jumla ya shilingi 4,117,000,000 kati ya shilingi 4,172,603,895 zilizotolewa, zimetumika .

**Skimu za Umwagiliaji maji Chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans – DADPs).***

**62. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2004/2005 skimu 52 zenye jumla ya hekta 7,947 ziliendelezwa katika Wilaya mbalimbali nchini. Uendelezaji wa skimu hizo ulifanyika chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Jumla ya shilingi 1,072,370,069 zilitumika.

## HIFADHI YA UDONGO NA MATUMIZI BORA YA ARDHI

**63. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi bora ya ardhi, hususan kilimo cha matuta, ujenzi wa makingamaji na upimaji wa mashamba kwa lengo la kuyamilikisha kwa wakulima. Jumla ya mashamba 3,602 yenye eneo la hekta 1,663 katika wilaya za Hai, Mpwapwa,

Bagamoyo na Singida Vijijini yalipimwa ili yamilikishwe kwa wakulima. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakulima kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali ya ardhi na sheria zinazosimamia sekta ya ardhi kwa wakulima 3,111 katika wilaya za Tarime, Geita, Songea, Morogoro, Singida, Kilosa, Mpwapwa, Kasulu, Kigoma, Muheza, Lushoto, Korogwe, Iringa na Shinyanga.

**64.** Aidha, jumla ya wakulima 196 katika skimu za umwagiliaji maji mashambani za Lumuma wilayani Kilosa na Mpwapwa na Kikafu Chini wilayani Hai, walipatiwa mafunzo juu ya kuzuia mmomonyoko wa udongo, hifadhi ya ardhi ya kilimo na udhibiti wa uharibifu wa miundo mbinu ya umwagiliaji maji mashambani. Upimaji wa mashamba ulifanyika katika skimu za Kikafu Chini, Hai (mashamba 720); Lumuma, Kilosa (mashamba 299); Lumuma, Mpwapwa (mashamba 240); Ruvu, Bagamoyo (mashamba 2,043); na Singida (mashamba 300). Aidha, wakulima wadogo 1,952 ambao wamepimiwa mashamba hayo wamepatiwa mafunzo juu ya hatimiliki ya kimila kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijiji za mwaka wa 1999.

**65.** **Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza uwajibikaji wa wananchi katika kutumia ardhi kwa njia endelevu, rasimu ya miongozo ya matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo imekamilika na imesambazwa kwa wadau mbalimbali ili waitolee maoni.

## HUDUMA ZA USHAURI WA KITAALAM

**66.** **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kutoa huduma za ugani kwa wakulima na wafugaji, hususan wanaoshiriki katika kutekeleza miradi iliyoko chini ya

Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Aidha, wakulima 670 walipatiwa mafunzo kuhusu kilimo bora cha zabibu, alizeti, karanga, mtama, viazi mviringo, mpunga, muhogo, uwele, mboga na matunda. Mafunzo mengine yalihusu hifadhi na usindikaji wa mazao na mbinu za kujikinga na UKIMWI. Mafunzo hayo yalifanyika katika vyuo vya wakulima vya Mkindo, Morogoro; Inyala, Mbeya; Bihawana, Dodoma na Ichenga, Njombe, ambavyo navyo viliimarishwa ili viweze kutoa mafunzo kwa kutumia mbinu shirikishi.

**67.** Aidha, vipindi 36 kuhusu kilimo bora cha mazao mbalimbali vilitayarishwa na kutangazwa na Redio Tanzania. Vipindi hivyo vilihusu kilimo bora cha mazao ya mboga, matunda, viungo, mbono, muhogo, mahindi na ngano. Vipindi kuhusu kilimo hai, wanyamakazi, hifadhi ya mazao, Sherehe za Nane Nane, umwagiliaji maji mashambani na athari za UKIMWI katika kilimo vilitangazwa. Vipeperushi kuhusu kanuni za kilimo bora cha mahindi, uvunaji wa maji ya mvua, matumizi bora ya mbolea, kilimo bora cha muhogo na viazi vitamu vilitayarishwa na kusambazwa kwa wakulima. Mikanda ya video kuhusu Siku ya Chakula Duniani, kilimo cha vanilla, paprika na mbono ilitayarishwa na kuonyeshwa kwa wakulima nchini na matoleo matatu ya gazeti la Ukulima wa Kisasa yalichapishwa na kusambazwa.

## UTAFITI WA KILIMO

**68.** **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kufanya utafiti ili kutoa teknolojia mbalimbali zitakazowawezesha wakulima kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji. Lengo lilikuwa kuzalisha na kukuza mbegu bora za mazao mbalimbali, kutoa teknolojia zenye lengo la kumuongezea mkulima mavuno, tija na faida, kubaini na kutathmini matatizo ya wakulima kwa kutumia mbinu shirikishi jamii na kuimarisha uwezo wa watafiti kutumia mbinu shirikishi katika kutathmini matatizo ya wakulima.

**69.** Katika mwaka wa 2004/2005, Vituo vya Utafiti vilitoa aina mpya sita za mbegu za mazao. Kituo cha Uyole kilitoa mbegu bora ya mahindi aina ya UH 6303, maharage aina ya Uyole 04 na BILFA na ngano aina ya SIFA. Kituo cha Kibaha kilitoa mbegu ya muhogo aina za Kiroba na Hombolo 95. Mbegu hizo zina sifa ya kutoa mavuno mengi zaidi na kuvumilia magonjwa. Ili kuhakikisha mbegu bora zinawafikia wakulima kwa haraka, jumla ya vipando milioni 1.5 vya muhogo vilizalishwa kwenye vituo vya Ukiriguru, Hombolo, Kibaha na Naliendele. Aidha, miche ya Migomba 30,000 ilizalishwa kwenye kituo cha Tengeru na jumla ya miche bora 2,284 ya matunda aina za maparachichi, papai na *passion* ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima.

**70.** Katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ilitumia shilingi bilioni 1.3 kuendesha shughuli za utafiti wa Kilimo katika kanda zote saba za utafiti wa kilimo zenye jumla ya vituo 17 ambavyo viko chini ya Wizara. Utafiti huo ulifanikiwa kuzalisha mbegu mpya kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na. 4.**

**71.** **Mheshimiwa Spika,** vituo vya Mlingano, Ilonga na Selian viliendelea kutafiti uwezo wa mazao ya jamii ya mikunde katika kuhifadhi na kuongeza rutuba ya udongo. Aina ya mikunde inayofanyiwa utafiti ni *Mucuna*, *Centrosema*, *Lablab*, *Stylosethes*, *Clitoria ternatea na Tropical kudzu*. Utafiti huo unaonyesha kuwa jamii hiyo ya mikunde ina uwezo wa kuongeza rutuba katika udongo na kudhibiti magugu katika sehemu nyingi zilizojaribiwa. Aidha, Kituo cha Mlingano kiliendelea kutayarisha ramani za mifumo ya kilimo ambapo ramani za kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa zinaandaliwa. Ramani hizo zitawasaidia watafiti kupendekeza teknolojia kulingana na kanda za ekolojia za kilimo.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuimarisha uwezo wa vituo vya utafiti na watafiti ambapo katika mwaka wa 2004/2005, makao makuu ya kanda za utafiti yaliyopo Uyole, Ukiriguru, Naliendele, Tumbi, Seliani, Ilonga na Mlingano viliunganishwa na mtandao wa *internet*. Vituo hivyo vimeunganishwa na maktaba inayohifadhi taarifa za matokeo ya utafiti duniani uitwao *The Essential Electronic Agricultural Library –TEEAL*. Kupitia mtandao huo watafiti watapata taarifa za utafiti unaofanywa na wenzao duniani. Aidha, Wizara imekamilisha ukarabati wa miundombinu ya utafiti na majengo katika vituo vya Uyole, Ilonga, Selian, Tumbi, Mlingano, Ukiriguru na Maruku na ukarabati wa maabara za bioteknolojia katika vituo vya Mikocheni, Uyole na Tengeru.

**UPATIKANAJI WA PEMBEJEO NA ZANA ZA KILIMO**

**73.** **Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa lengo la kupanua soko, matumizi na kuhakikisha kuwa zina ubora unaotakiwa. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 195,065 za mbolea zilipatikana, kati ya hizo, tani 81,766 ziliuzwa chini ya utaratibu wa ruzuku. Aidha, jumla ya tani 15,239.50 za madawa ya unga na lita milioni 1.8 za madawa ya maji zilipatikana. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 12,830.58 za mbegu bora za mazao zilipatikana na kutumiwa nchini, kati ya hizo, tani 3,758.12 zilizalishwa nchini.

**74.** Mwaka wa 2004/2005, jumla ya matrekta makubwa na madogo 429, plau 80,761 na majembe ya mkono milioni 1.98 yaliingizwa nchini. Kati ya hayo, matrekta 29 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.182 yalinunuliwa kupitia mikopo ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo. Matrekta 98 yalikarabatiwa kwa kugharamiwa na mikopo iliyotolewa na Mfuko huo. Vituo 20 vya wanyamakazi vilifanyiwa ukarabati na maofisa ugani 456 wamepatiwa mafunzo kuhusu wanyamakazi (**Kiambatisho Na.5**). Aidha, Wizara imeiwezesha sekta binafsi, kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, kuanzisha vituo viwili vya kukodisha matrekta katika

wilaya za Masasi na Kilombero.

**Mbolea, Madawa na Mbegu Bora**

**75. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005 ilikadiriwa kuwa mahitaji ya mbolea nchini yatakuwa tani 385,000. Hadi tarehe 13 Aprili, 2005, jumla ya tani 195,065 za mbolea sawa na asilimia 50.66 ya mahitaji zilikuwa zimepatikana. Kiwango hicho ni sawa na ogezeko la asilimia 55.25 ikilinganishwa na upatikanaji wa mbolea katika mwaka wa 2003/2004.

**76. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 7.244 kwa ajili ya kugharamia utaratibu wa ruzuku kwenye mbolea. Kiasi hicho cha fedha kilikadiriwa kugharamia jumla ya tani 81,766 za mbolea aina za DAP, Urea, CAN, TSP na NPK. Hadi tarehe 15 Juni, 2005, jumla ya tani 73,569.33 za mbolea hizo, sawa na asilimia 90.0 ya lengo zilikuwa zimesambazwa na kutumiwa na wakulima. Aidha, jumla ya shilingi 7,244,000,000 zilitumika kugharamia utaratibu huo.

**Madawa**

**77. Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya viuatilifu katika mwaka wa 2004/2005 yalikuwa tani 21,000 za madawa ya unga na lita milioni 4.0 za madawa ya maji. Upatikanaji ulikuwa tani 15,239.5 za madawa ya unga na lita 1,801,776 za madawa ya maji. Viwango hivyo havikufikia lengo, hususan kwa madawa ya korosho ambapo mahitaji yalikuwa tani 8,549 lakini zilipatikana tani 5,132 kutokana na waagizaji kuhofia ukame. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imeanza kutekeleza utaratibu wa kutoa ruzuku, ambapo lita 30,814 za madawa ya maji na tani 474 za madawa ya unga zitagharamiwa sehemu ya bei na gharama za usafirishaji. Aidha, jumla ya shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya ruzuku

ya madawa ya korosho na shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukarabati wa mabomba ya kupulizia madawa hayo.

**Mbegu Bora**

**78.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, upatikanaji wa mbegu bora za mazao ulikadiriwa kuwa tani 13,300, ambapo jumla ya tani 12,830.58 za mbegu hizo zilipatikana. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 96.50 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, mashamba ya mbegu ya Serikali na Vituo vya Utafiti vilizalisha tani 1,010.41 na wakulima wadogo vijijini tani 426.39. Makampuni binafsi ya mbegu nchini yalizalisha jumla ya tani 2,747.71 ya mbegu za mazao ya chakula na tani 2,732.9 za mbegu za pamba. Aidha, tani 6,571.65 za mbegu za mazao mbalimbali ya chakula ziliagizwa kutoka nje ya nchi.

**79.** Ili kuhakikisha mbegu zinazozalishwa au kuingizwa nchini zina ubora unaotakiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni, ukaguzi wa mbegu ulifanyika katika mashamba yanayozalisha na maghala yanayohifadhi mbegu. Aidha, mbegu zinazoingizwa kutoka nje zilikaguliwa mipakani. Jumla ya sampuli 1,563 za mbegu zilipimwa ubora katika maabara za Taasisi ya Ukaguzi na Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (*Tanzania Official Seed Certification Institute - TOSCI*). Kati ya hizo, sampuli 30 hazikufikia kiwango cha ubora na hivyo kuzuiwa kuingia katika soko. Aidha, kampuni moja ya mbegu imefikishwa mahakamani kwa kuuza mbegu ambazo haimiliki kisheria, hivyo kukiuka sheria na kanuni za biashara za mbegu.

**80.** **Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2004/2005, Kamati ya Taifa ya Kuruhusu Matumizi ya Aina Mpya za Mbegu iliruhusu jumla ya aina 11. Kati ya hizo, aina sita za mbegu zilizalishwa katika vituo vya utafiti vilivyopo chini ya Wizara na tano kutoka mashamba ya makampuni ya mbegu. Aina za mbegu zilizopitishwa

ni Mahindi aina za UH 6303, ETA 102, ETA 34, na Longe 6H; ngano aina ya UW 90028; maharage aina za Uyole 98 SPS na BILFA 16; muhogo aina za Kiroba na Hombolo 95 na Shairi aina za Karne na 9831.

**Zana za kilimo**

**81. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kuhimiza matumizi ya zana bora za kilimo nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya matrekta makubwa 272, matrekta madogo 157, majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 80,761 na majembe ya mkono 1,989,218 yaliingizwa nchini. Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wake wa kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu matumizi ya wanyamakazi. Mwaka wa 2004/2005 vituo 20 vilivyopo katika Halmashauri za Ludewa, Njombe, Kilolo, Ileje, Kyela, Magu, Bunda, Singida vijijini, Manyoni, Iramba, Singida mjini, Tanga mjini, Lushoto, Tabora mjini, Mtwara mjini, Mpwapwa, Mvomero, Mbinga, Kigoma na Biharamulo vilitoa mafunzo hayo. Wakulima 1,180 walipatiwa mafunzo ya kilimo cha maksai na matumizi ya zana za wanyamakazi kupitia vituo hivyo. Aidha, vituo hivyo vimepatiwa zana za kufundishia wakulima kilimo cha wanyamakazi kwa kutumia majembe aina ya ripa, tindo, majembe ya palizi na kupigia matuta na mashine za kupandia.

**82. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kutoa mafunzo kuhusu matumizi na matengenezo ya matrekta madogo ya mkono ambapo jumla ya Maafisa Zana 25 kutoka wilaya za Kigoma, Kasulu, Kibondo, Muleba, Biharamulo, Magu, Geita, Sengerema, Misungwi, Kahama, Musoma, Tabora Mjini, Uyui, Urambo, Nzega, Igunga, Iramba, Singida Vijijini, Manyoni, Sumbawanga Mjini, Mbarali, Korogwe, Handeni na Moshi Vijijini walipewa mafunzo. Aidha, wakulima 269 na maofisa ugani 30 kutoka mikoa ya Mtwara, Pwani, Lindi, Ruvuma, Iringa na Tanga walipatiwa mafunzo ya matumizi ya mashine ndogo za kubangua korosho.

## MFUKO WA TAIFA WA PEMBEJEO

**83. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 3,631,075,000. Mikopo hiyo ilitumika kugharamia kununua matrekta mapya na kukarabati matrekta mabovu na ununuzi wa pembejeo za kilimo na mifugo. Pembejeo zilizonunuliwa ni pamoja na tani 3,693 za mbolea, tani 7,916 na lita 23,634 za madawa ya mimea, lita 15,074 za madawa ya mifugo, tani 1,254 za vyakula vya mifugo, vifungashio vya mazao 37,932, zana ndogo ndogo 1,772 na tani 88 za mbegu. Aidha, Mfuko ulitoa mikopo ya kununulia matrekta mapya 33 na kukarabati matrekta 112. Kuanzia mwaka wa 2002/2003, hadi mwaka wa 2004/2005 mikopo yenye thamani ya shilingi 9,663,446,678.00 imetolewa kupitia benki mbalimbali na Shirikisho la Vyama vya Kuweka na Kukopa (SCCULT). Mchanganuo wa mikopo iliyotolewa na marejesho umeainishwa kwenye **(Kiambatisho Na.6)**.

**84. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa uliendelea kukusanya madeni yenye thamani ya shilingi bilioni 5.8 yaliyotolewa katika kipindi cha mwaka wa 1995/1996 hadi 1998/1999. Hadi mwezi wa Mei, 2005, jumla ya shilingi bilioni 4.45 zilikuwa zimerejeshwa. Hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kukusanya madeni yaliyobaki.

## MAFUNZO YA KILIMO KWA WATAALAM NA WAKULIMA

**85. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, vyuo vya kilimo vinavyosimamiwa na Wizara vilikuwa na jumla ya wanafunzi 844 **(Kiambatisho Na. 7)**. Kati ya hao, wanafunzi 400 wanagharamiwa na Serikali na wanafunzi 444

wanajigharamia wenyewe**.** Katika kipindi hicho, wataalam 81 wa kilimo walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, wanawake walikuwa 23 na wanaume 46. Aidha, watumishi watatu wanahudhuria mafunzo ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kilimo Cha Sokoine (SUA) na wawili wanahudhuria mafunzo ya shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu Huria.

**Mafunzo kwa Vitendo katika Vyuo vya Kilimo**

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka miwili ambapo wanafunzi huwa chuoni, hutumia asilimia 40 ya muda wao kujifunza nadharia na asilimia 60 kujifunza kwa vitendo. Ili kuwaimarisha wanafunzi katika mafunzo ya vitendo, katika mwaka wa 2004/2005, wanafunzi walilima jumla ya hekta 651 za mazao mbalimbali ya nafaka, mikunde, pamba na alizeti. Aidha, wanafunzi hao walifuga jumla ya ng'ombe wa maziwa 216, mbuzi 49, kondoo 87, nguruwe 133, punda 25, kuku 1,768 na wanyamakazi 26 **(Kiambatisho Na. 8**).

**Mafunzo kwa Wakulima**

**87. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2004/2005, vyuo vya kilimo vya Serikali vilitoa mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima 8,749. Kati ya hao wanawake walikuwa 3,953 na wanaume 4,796. Chuo cha *Kilimanjaro Agricultural Training Centre (KATC*), kinachofundisha kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji maji mashambani, kilifundisha wakulima 1,641. Kati ya hao, wanafunzi 583 walitoka nchi jirani za Kenya, Uganda, Malawi na Zambia. Chuo cha Taifa cha Sukari, Kidatu kilifundisha wakulima 179 kuhusu kilimo bora cha miwa. Wakulima wengine 6,929 walipatiwa mafunzo katika vyuo vya Igurusi (wakulima 4,650), Uyole (1,007), Mlingano (628), Ukiriguru (314), Mtwara (288) na Ilonga wakulima (42). (**Kiambatisho Na. 9).** Mafunzo hayo

yaligharimu shilingi 239,983,720.

**Ukarabati wa Vyuo vya Mafunzo**

**88. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za kuboresha mazingira ya kuendesha mafunzo ya wataalam na wakulima vyuoni, Wizara iliendelea kukarabati majengo 30 ya vyuo. Miundo mbinu ya maji na umeme imekarabatiwa katika vyuo vya Tumbi na Ukiriguru. Wizara ilinunua vifaa vya mafunzo kwa vitendo, hususan vifaa vya maabara na karakana. Aidha, matrekta matatu na zana zake yalinunuliwa kwa ajili ya vyuo vya Igurusi, Mlingano na Mtwara.

## HIFADHI NA USALAMA WA CHAKULA

**Hifadhi ya Chakula ya Taifa**

**89. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa 2004/2005, Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilipanga kununua tani 100,000 za mahindi na tani 1,000 za Mtama kupitia Kanda zake sita zilizoko Makambako, Songea, Sumbawanga, Shinyanga, Arusha na Dodoma. Ilikadiriwa kwamba shilingi bilioni 12.33 zingehitajika kugharamia ununuzi huo. Hadi mwezi wa Mei 2005, jumla ya tani 97,401 za mahindi zilikuwa zimenunuliwa na kufanya akiba ya chakula katika Hifadhi ya Taifa kuwa tani 120,000. Ununuzi wa mtama haukufanyika kwa sababu haukupatikana.

**Ukusanyaji wa takwimu za mvua na hali ya chakula**

**90. Mheshimiwa Spika**, Ili kuwa na uwezo wa kukusanya taarifa sahihi na katika muda unaotakiwa, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kuimarisha uwezo wa vituo vyake ambapo, jumla ya vituo 100 vilipatiwa vifaa vya kukusanya takwimu za upatikanaji wa mvua, hali ya mazao mashambani na kiasi cha mavuno yanayotegemewa. Aidha, tathmini ya hali ya upatikanaji wa

mazao ya chakula mashambani ilifanyika katika mikoa 20 ili kutambua maeneo ambayo yanakabiliwa na upungufu wa chakula kwa ajili ya kutafutiwa msaada.

**Hifadhi ya mazao na usalama wa chakula**

**91. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ilianza kutekeleza kampeni ya kuhimiza hifadhi bora ya mazao baada ya mavuno na kueleimisha wakulima mbinu za kukadiria kiwango cha chakula kitakachokidhi mahitaji ya kaya, kuanzia baada ya mavuno hadi mavuno mengine yatakapopatikana. Lengo la kampeni hiyo ni kuwajengea uwezo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayokabiliwa na hali ya ukame wa mara kwa mara ili wakabiliane na matatizo ya upungufu wa chakula.

**92.** Kuanzia mwezi wa Novemba, 2004 hadi Mei, 2005, kampeni hiyo ilifanywa katika Halmashauri za wilaya 49 za mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mwanza, Mara, Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro na Arusha. Nakala 23,000 za miongozo ya ukadiriaji na hifadhi ya chakula kwa wakulima zilitayarishwa na kutolewa kwa wakulima. Aidha, maafisa ugani 1,712 kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mwanza, Mara, Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro na Arusha walipatiwa mafunzo ya mbinu bora ya hifadhi ya mazao baada ya mavuno.

## UDHIBITI WA VISUMBUFU VYA MIMEA NA MAZAO YA KILIMO

**93. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ilidhibiti milipuko ya visumbufu vya mazao ya wakulima mashambani kama ifuatavyo:-

- *Quelea quelea* katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Shinyanga na Mwanza. Makundi ya ndege wapatao milioni 65 waliokuwa wanashambulia mazao ya wakulima yaliangamizwa kwa kutumia lita 1,944 za dawa ya kudhibiti ndege hao. Mazao mengi ya wakulima yaliokolewa katika mikoa hiyo ikiwa ni pamoja na maeneo mengine ambayo yangeshambuliwa iwapo ndege hao wasingedhibitiwa;

- Viwavijeshi katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma na Kilimanjaro ambapo lita 4,500 za dawa za wadudu zilitumika kupulizia hekta 1,593 za mazao ya nafaka. Aidha, mitego 78 ya kukusanya taarifa za kutabiri milipuko ya viwavijeshi ilifanyiwa ukarabati na lita 32,000 za madawa ya visumbufu zilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kanda vya udhibiti wa visumbufu kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya viwavijeshi mara itakapotokea;

- Eneo la hekta 14,000 katika mbuga za Iku/Katavi, ziwa Rukwa, Wembere, mabonde ya mito Malagarasi na Bahi mkoani Dodoma yalinyunyuziwa lita 7,450 za sumu na kuwaangamiza nzige hao kabla hawajaruka na kushambulia mazao mashambani;

- Milipuko ya panya ilidhibitiwa katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Morogoro, Mbeya na Kilimanjaro ambapo kilo 59,055 za sumu ya panya zilitumika. Wakulima 8,850 walipewa mafunzo ya udhibiti husishi wa panya mashambani.

- Uzalishaji na usambazaji wa mbawakavu kwa ajili ya udhibiti wa gugumaji katika Ziwa Viktoria na mabonde ya mito Mara na Kagera uliendelea kutekelezwa. Aidha, Wizara iliendelea kutekeleza mpango wa kudbibiti

mashambulizi ya funza wa mabua ya nafaka kwa kumtumia mdudu adui wa funza hao aitwae *Cortesia flavipes.* Katika mwaka wa 2004/2005, Taasisi ya Udhibiti wa Visumbufu Kibiolojia iliyopo Kibaha, Pwani ilizalisha wadudu maadui wa funza hao *(Cortesia flavipes)* wapatao 1,000,000 na kuwasambaza katika mikoa ya Pwani, Tanga, Dodoma, Morogoro, Kilimanjaro, Arusha na Mara.

**Utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea (*Plant Protection Act, 1997*)**

**94. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kutekeleza Sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao ya mwaka wa 1997. Kuanzia mwezi wa Julai, 2004 hadi Juni, 2005, tani 681,043.15 za bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo yaliyosafirishwa nje ya nchi yalikaguliwa. Katika kipindi hicho, tani 1,173,466.7 za mimea na mazao yake yaliyoingizwa nchini yalikaguliwa usafi na afya kwa nia ya kuzuia visumbufu vilivyo katika karantini visiingizwe nchini. Jumla ya vyeti vya usafi 4,274 na vibali 200 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa. Aidha, ili kuhakikisha viuatilifu vinavyoingizwa nchini vina ubora na ufanisi unaotakiwa kwa mujibu wa sheria, vibali 271 vya uingizaji viuatilifu vilitolewa kwa makampuni mbalimbali.

## UBINAFSISHAJI WA MASHAMBA NA MASHIRIKA YA KILIMO

**95. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma kubinafsisha mali za Shirika la Kilimo na Chakula (NAFCO), Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC), Mamlaka ya Mkonge Tanzania (TSA), Bodi ya Korosho na Bodi ya Kahawa. Ubinafsishaji huo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

### Ubinafsishaji wa Mashamba ya NAFCO

**96.** Serikali iliruhusu shamba la mpunga la Ruvu libinafsishwe kwa wakakulima wadogo. Wakulima wameunda Chama cha Ushirika (CHAURU). Shamba hilo limepimwa na kugawanywa katika mashamba ya ekari mbili mbili ambayo yamemilikishwa kwa wakulima wadogo 820. Aidha, shamba la mpunga

la Dakawa limekabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ili ligawanywe kwa wakulima. Shamba la mahindi la Mbozi litamilikishwa kwa mwekezaji aliyeshinda zabuni, mara atakapolipia asilimia 50 ya bei ya mauzo na kutia saini Mkataba wa Mauzo. Hivi sasa mwekezaji huyo amekwishalipa asilimia kumi ya bei ya mauzo.

**97.** Katika mwaka wa 2004/2005, Serikali ilitangaza kuuzwa kwa shamba la mahindi la Namtumbo. Hata hivyo, wawekezaji waliojitokeza hawakufikia viwango vilivyowekwa. Hali hiyo imelazimu shamba hilo litangazwe tena. Aidha, upimaji wa mashamba ya ngano ya West Kilimanjaro ya Journey’s End, Fosters, Matadi, Harlington na Kanamondo umekamilika na mashamba hayo yametangazwa kuuzwa. Uamuzi wa kubinafsisha mashamba ya Mbarali na Kapunga upo katika hatua za mwisho kutolewa. Aidha, kuhusu ubinafsishaji wa mashamba ya ngano ya Gawal na Warret, iliamuliwa yaondolewe kwenye kundi la mashamba ya Hanang yatakayobinafsishwa ili yagawiwe kwa wananchi wanaoishi jirani na mashamba hayo. Kutokana na madeni ya mashamba hayo kuwa makubwa, imeamuliwa mashamba yaliyobakia yafilisiwe kupitia Wakala wa Ukusanyaji wa Madeni ya Mashirika ya Umma na Serikali *(LART)* kwa masharti kwamba mashamba hayo yasigawanywe.

**Ubinafsishaji wa Viwanda na Mali za Mashirika ya Umma Mbalimbali**

**98.** **Mheshimiwa Spika**, ubinafsishaji wa viwanda 12 vya Korosho upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Viwanda vya Newala I, Newala II, Kibaha, TANITA I, Masasi, Lindi na Likombe vimepata wanunuzi na utaratibu wa kuvikabidhi kwa wanunuzi hao unaendelea. Viwanda vya TANITA II, Mtwara, Mtama na Nachingwea ambavyo havikupata wawekezaji katika matangazo ya awali, vilitangazwa tena kuuzwa mwezi wa Februari, 2005 na kupata wawekezaji. Taratibu za ubinafsishaji wa viwanda hivyo zinaendelea. Kiwanda cha Tunduru bado hakijapa mwekezaji na kitatangazwa tena.

**99.** **Mheshimiwa Spika,** ubinafsishaji wa Kiwanda cha Kahawa cha Kagera (TANICA) umekamilika. Katika ubinafsishaji huo Serikali imeuza asilimia 54.53 ya hisa zake kwa Vyama vya Ushirika vya Kagera na Karagwe. Asilimia 10 ya

hisa za Serikali itaendelea kumilikiwa na Serikali ili baadaye ziuzwe kwa wawekezaji. Serikali ilibinafsisha vinu vya mpunga vya Isaka, Tabora na Shinyanga na kinu cha mahindi cha Mzizima (Plot No. 33) vilivyokuwa vinamilikiwa na Shirika la Usagishaji la Taifa.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mikataba kati ya Serikali na wawekezaji walionunua mashamba na viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na mashirika mbalimbali ya umma yaliyoko chini ya Wizara. Katika kufanya hivyo, iligundulika kuwa wawekezaji kwenye kiwanda na shamba la chai cha Dabaga, Iringa na mali za NMC zilizoko Mwanza walishindwa kutekeleza mikataba ya mauzo. Serikali ilisitisha utekelezaji wa mikataba hiyo na kuzirejesha PSRC mali zilizokuwa zimebinafsishwa ili zitangazwe upya na kuuzwa kwa wawekezaji wenye uwezo na nia ya kuziendeleza.

**101. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mkataba kati ya Serikali na Kampuni ya *M/s. Katani Ltd.*, kuhusu ubinafsishaji wa baadhi ya mashamba ya mkonge yaliyokuwa yanamilikiwa na Mamlaka ya Mkonge, utaanza tena baada ya makubaliano mapya ya ubinafsishaji kati ya pande mbili kufikiwa. Chini ya makubaliano hayo, Kampuni ya *M/s Katani Ltd.* itarejesha Serikalini mashamba yote manane ya mkonge waliyouziwa ili yabinafsishwe upya kwa wawekezaji mbalimbali, wakiwemo wakulima wadogo ambao tayari wamekodishiwa sehemu za mashamba hayo. Aidha, kiwanda cha kamba cha *Tanzania Cordage Ltd.* (TANCORD), majengo na karakana zake yatabinafsishwa kwa Kampuni ya *M/s. Katani Ltd*.

## KUREKEBISHA NA KUHUISHA SERA NA SHERIA

### Uhuishaji wa Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka wa 1997

**102. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ilianza kuhuisha Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka wa 1997 ili kuiwezesha itoe maelekezo ya kisera ya kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA), Mkakati wa Maendeleo Vijijini *(Rural Development*

*Strategy –RDS),* Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy* - *ASDS)* na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme* - *ASDP).* Aidha, Wizara ilikamilisha rasimu ya Sera ya Chakula ambayo itachapishwa mara baada ya kupitishwa na Serikali**.** Wizara pia imeanza kufanya uchunguzi utakao wezesha kutungwa kwa sheria mpya za kilimo na kuhuisha zile zilizopo ili zitumike kutekeleza sera hizo mara zitakapopitishwa na Serikali.

**Urekebishaji na Utekelezaji wa Sheria za Kilimo**

**103. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali zilizoko chini yake na kuwachukulia hatua za kisheria wakiukaji. Wizara pia ilikamilisha maandalizi ya rasimu ya muswada wa sheria ya mbolea na kuijadili na wadau wa sekta ya kilimo. Muswada huo utawasilishwa Bungeni baada ya kupitishwa katika ngazi mbalimbali za Serikali. Uchunguzi utakaowezesha kutungwa kwa Sheria ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani na kuhuisha Sheria za Kudhibiti Visumbufu vya Mimea na Mazao (*The Plant Protection Act, 1997),* Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu (*"The Tropical Pesticides Research Institute Act, 1979")* na Sheria ya Usalama wa Chakula (*Food Security Act No.10 of, 1991*) ulikamilishwa. Wizara ilikamilisha maandalizi ya Kanuni za Sukari, Tumbaku, Korosho na Pamba ambazo zitaanza kutekelezwa katika mwaka 2005/2006 baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Aidha, Serikali ilikamilisha tathmini ya miundo na majukumu ya taasisi zilizo katika sekta ya kilimo ili kubaini utaratibu utakaoziwezesha kutoa huduma kwa wadau kwa ufanisi zaidi.

**104. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa 2004/2005, Wizara ilianzisha rasmi Ofisi ya Msajili wa wagunduzi wa Mbegu Mpya za Mimea (*Plant Breeders Rights Registry*). Msajili wa Haki Miliki za Wagunduzi na Watafiti wa Mbegu Mpya za Mimea aliteuliwa na kuanza kazi. Aidha, ofisi ya Msajili ilikarabatiwa na vitendea kazi vilinunuliwa ili kumwezesha asimamie utekelezaji wa Sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi na Watafiti wa Mbegu Mpya za Mimea na Mazao ya mwaka wa 2002 (*The Plant Breeders' Rights Act, 2002*). Kupitia Sheria hiyo,

Wizara ilikamilisha taratibu za awali za kusajili aina saba (7) za mbegu ambazo ziligunduliwa na watafiti walioajiriwa na Serikali katika vituo mbalimbali vya utafiti.

**Sensa ya Kilimo na Mifugo**

**105. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2004/2005 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, iliendelea kuchambua takwimu za sensa ya kilimo na mifugo iliyofanyika mwaka wa 2003/2004. Ripoti ya kitaifa ya sensa hiyo inatarajiwa kutolewa mwezi wa Juali, 2005.

**MAENDELEO YA WATUMISHI**

**106. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2004/2005, Wizara iliendelea na zoezi la kupandisha vyeo na kurekebisha ajira za watumishi wake. Jumla ya watumishi 1,474 walipandishwa vyeo wanavyostahili, baada ya kufanyiwa upekuzi na kuonekana kuwa hawana dosari za kimaadili. Idadi hiyo inafanya jumla ya watumishi waliopandishwa kati ya mwaka wa 2000/2001 na 2004/2005 kufikia watumishi 2,564. Aidha, watumishi 392 walithibitishwa kazini, watumishi 77 walirekebishiwa ajira zao na watumishi 46 waliajiriwa kwa mara ya kwanza katika utumishi wa umma. Wizara pia ilitoa mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi ya fomu za wazi za mapitio na upimaji utendaji kazi (OPRAS) na kuhusu lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

## KAZI ZITAKAZOFANYIKA NA MATARAJIO YA MWAKA WA 2005/2006.

**107. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2005/2006, utakuwa mwaka wa nne wa utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP).* Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu hiyo katika maeneo yaliyo chini yake. Aidha, Programu hiyo itaendelea kuwa chombo cha kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) katika sekta ya kilimo, hususan kundi (*cluster)* la kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Asilimia 95.6 ya maombi ya fedha ya bajeti ya Wizara itatekeleza MKUKUTA kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo.

## PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO

**108. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Idara, Vitengo, Taasisi na Asasi zilizoko chini ya Wizara zitajielekeza katika kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Taasisi hizo, hususan zile zinazosimamia uendelezaji wa mazao, zimeandaa mipango ya maendeleo ya mazao, ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Aidha, miradi yote iliyoko katika ngazi ya Taifa, italenga katika kuvipatia ufumbuzi vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo.

### Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs)

**109. Mheshimiwa Spika**, mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs), ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Hivyo, ni muhimu Wilaya zote kuhakikisha zinaandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya na kuihuisha kila mwaka ili kuhakikisha wakulima wanajiwekea malengo ya muda mrefu na mfupi ya kukuza uchumi katika maeneo yao na kujiondolea umaskini. Miradi yote ya kilimo katika ngazi za Wilaya itapaswa kujielekeza katika kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya kama sehemu muhimu ya utekelezaji wa MKUKUTA katika

ngazi ya Wilaya. Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali itaendelea kutekeleza DADPs. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango hiyo.

**110.** Katika mwaka wa 2005/2006 Miongozo ya Kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya iliyoandaliwa katika mwaka wa 2004/2005 itaanza kutumika katika kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya zote. Timu za uwezeshaji wilaya ambazo zitazisaidia wilaya katika kuandaa mipango hiyo, zimeelimishwa umuhimu wa kuzingatia miongozo hiyo. Aidha, katika kuibua miradi itakayotekelezwa chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, Wilaya zinashauriwa kuzingatia malengo ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, hususan yaliyoainishwa katika Mpango wa Utekelezaji wa Programu hiyo wa mwaka 2005/2006, ambao nauwasilisha leo.

### Mpango wa Wizara wa Kutekeleza Programu ya Sekta ya Kilimo

**111. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Mpango wa Wizara wa kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo unalenga katika kuendeleza na kuimarisha juhudi ambazo zilianzishwa katika miaka mitatu iliyopita ya utekelezaji wa Programu kwa:-

- kuhimiza uzalishaji wa mazao ya kilimo utakaoliwezesha Taifa kujitosheleza kwa chakula na kuwa na hifadhi ya kutosha katika ngazi ya kaya na Taifa;
- kutekeleza mikakati itakayoongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji maji mashambani;
- kuhimiza uzalishaji, tija na ubora wa mazao ya biashara ili kukiwezesha kilimo kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi na kuondoa umaskini;
- kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mifumo madhubuti ya upatikanaji wa pembejeo na zana bora na za kutosha na kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvunwa; na
- kuimarisha usindikaji wa mazao na huduma za utafiti na ugani.

**112. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo inatekelezwa kama ilivyopangwa, Wizara kupitia Kitengo cha Kuratibu Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- Kuhamasisha wadau wote kuhusu Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wadau wayaelewe malengo ya Programu na utaratibu wa utekelezaji wake;
- Kuainisha na kuweka utaratibu wa kutekeleza masuala yanayohitaji utekelezaji wa haraka, ambayo utekelezaji wake utawezesha malengo ya muda mrefu na wa kati ya Progamu yafikiwe;
- Kuratibu uibuaji na uandaaji wa miradi na mipango katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha kuwa miradi na mipango hiyo inajielekeza katika kutekeleza Programu;
- Kuongoza malengo na kazi za miradi ya kilimo inayoendelea kutekelezwa katika ngazi za Taifa na Wilaya ili ijielekeze katika kutekeleza dhumuni kuu (*mission*) na dira (*vision*) ya Programu;
- Kuendelea kuratibu uandaaji, ufadhili na utekelezaji wa mipango ya kilimo ya Taasisi, Asasi na Wilaya inayolenga katika kutekeleza Programu, ikiwemo Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans - DADPs*); na
- Kukamilisha na kufuatilia utekelezaji wa taratibu za uchangiaji kwenye Kapu la Kufadhili Mipango ya Sekta ya Kilimo katika ngazi ya Taifa na Wilaya (*Basket Funding*).

**Kuhuisha Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997**

**113.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itakamilisha kazi ya kuhuisha Sera ya Kilimo na Mifugo iliyoanza kuhuishwa mwaka wa 2004/2005. Kazi kubwa itakayofanyika ni kuwashirikisha wadau kujadili rasimu ya Sera hiyo kabla ya kuiwasilisha Serikalini.

**Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji**

**114. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendelea kutekeleza Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji katika wilaya 29 za Tanzania Bara na Wilaya tano za Zanzibar zilizoanza kutekeleza mradi huo kuanzia mwaka wa 2003/2004. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na :-

- Kuwezesha wilaya zinazotekeleza mradi kutekeleza miradi midogo 1,001 iliyoibuliwa na kuandaliwa mwaka wa 2003 hadi 2005;
- Kuwezesha jamii katika wilaya zinazohusika kubuni na kutekeleza miradi 1,170 mipya itakayoibuliwa katika mwaka wa 2005/2006 katika vijiji hivyo;
- Kutoa mafunzo ya mbinu shirikishi kwa wawezeshaji wa Taifa, wilaya na kata ili kuwajengea uwezo wa kushirikisha jamii katika kupanga mipango ya kuendeleza kilimo na ufugaji;
- Kuwezesha uhuishaji wa Sera za Kitaifa, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zikiwemo ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maendeleo ya kilimo.

**Programu ya Huduma za Kilimo *(Agricultural Services Support Program - ASSP)***

**115. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006 Wizara itaanza kutekeleza Programu ya Kuboresha Huduma za Kilimo yenye lengo la kufanikisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima kupitia vikundi. Kazi za awali katika utekelezaji wa programu hiyo ni uwezeshaji wa wakulima, kupitia vikundi vyao, kwa kuwapatia elimu na uwezo wa kubaini na kuomba kupatiwa huduma na teknolojia wanazohitaji. Utoaji huduma za ugani utaimarishwa kwa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi. Aidha, mfumo wa kuendesha utafiti utarekebishwa ili uzingatie zaidi mahitaji ya walengwa. Kazi kubwa itakayofanyika mwaka wa 2005/2006, ni kuimarisha uwezo wa walengwa ili kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa malengo ya mradi.

**Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agricultural Sector Investment Project - DASIP)***

**116. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006 Wizara za Sekta ya Kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaanza kutekeleza Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani katika wilaya zote za mikoa ya Mara, Mwanza, Shinyanga, Kigoma na Kagera. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na:-

- Kuzindua mradi katika wilaya 25 zitakazoanza kutekeleza mradi katika mwaka wa 2005/2006, ikiwa ni pamoja na kuunda timu za wawezeshaji za wilaya na kata na kujenga uwezo wa kuandaa miradi, kufuatalia utekelezaji, usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha;
- Kuandaa vikundi vya wakulima, wafugaji na kuendesha mafunzo ya mbinu shirikishi jamii katika kupanga mipango ya kuendeleza kilimo na ufugaji;
- Kuwezesha jamii katika wilaya 25, kuibua, kuandaa na kutekeleza miradi midogo ya kilimo na ufugaji.

## UENDELEZAJI WA MAZAO MAKUU YA BIASHARA

**117. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kuratibu na kusimamia Mipango ya Maendeleo ya Mazao makuu ya biashara ambayo ni chai, kahawa, korosho, katani, pamba, pareto, sukari na tumbaku. Aidha, Wizara kupitia Bodi za Mazao, itahakikisha uzalishaji, tija na ubora wa mazao unaongezeka ili kukabiliana na ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa uuzaji wa mazao ya biashara unafanyika kwa kufuata madaraja, vipimo na katika vituo vilivyoidhinishwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo. Matarajio ya uzalishaji wa mazao makuu ya biashara katika msimu wa 2005/2006 ni kama ifuatavyo:-

**Chai**

**118. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 4.1 kutoka tani 32,000 zilizozalishwa mwaka wa 2004/2005 hadi tani 33,300 katika msimu wa 2005/2006. Ongezeko hilo litatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chai katika maeneo mapya ya wilaya za Njombe, Mufindi, Muheza na Lushoto yaliyopandwa chai msimu 2003/2004 na ufufuaji wa mashamba ya chai ya wakulima wadogo yaliyokuwa yametelekezwa, yenye ukubwa wa hekta 115 katika wilaya ya Njombe; hekta 500, Bukoba na hekta 100, Muleba. Kuanza kwa uzalishaji wa mashamba ya Kyimbila na Rungwe yaliyokuwa ya *George Williamson (T) Limited* baada ya kuuzwa kwa *Wakulima Tea Company,* nako kunatarajiwa kuongeza uzalishaji. Aidha, bei nzuri ya chai kwa msimu uliopita inatarajiwa kuongeza tija na uzalishaji, hususan kwa wakulima wadogo.

**Kahawa**

**119. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, uzalishaji wa kahawa unatarajiwa kushuka kutoka tani 54,000 zilizozalishwa mwaka wa 2004/2005 hadi tani 45,000, sawa na upungufu wa asilimia 17.7. Upungufu huo utatokana na tabia ya mzunguko wa uzalishaji wa zao la kahawa ambao hupanda na kushuka mwaka unaofuata. Mwaka wa 2005/2006 utakuwa mwaka wa kushuka kwa uzalishaji kahawa katika mzunguko huo. Hata hivyo, inatarajiwa kwamba bei za kahawa zitapanda na hivyo kuwezesha mapato yatakayotakana na mauzo kutoshuka, yakilinganishwa na mapato ya mwaka wa 2004/2005. Kutoshuka kwa mapato ya mauzo kutatokana na kuongezeka kwa ubora wa kahawa inayouzwa nje moja kwa moja, bila kupitia mnadani. Inatarajiwa pia kwamba, viwanda vya kupukuchulia kahawa vilivyojengwa na kukarabatiwa mwaka wa 2004/2005 vitaongeza ubora wa madaraja na mionjo ya kahawa, kulingana na viwango na mahitaji ya soko la kimataifa.

**Katani**

**120. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006 uzalishaji wa katani unatarajiwa kufikia tani 30,000 kutoka tani 26,800, zilizozalishwa mwaka wa

2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 12. Ongezeko hilo litatokana na kuongezeka kwa eneo lililopandwa mkonge kwa hekta 7,458 zitakazoanza kukatwa mkonge uliolimwa kati ya miaka ya 1999/2000 na 2001/2002, mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na *M/s Katani Ltd.* yataanza kuzalisha mkonge baada ya kubinafsishwa upya na uzalishaji wa mkonge kwa wakulima wadogo katika Kanda ya Ziwa utaongezeka. Aidha, uzalishaji wa katani utaongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya katani katika masoko ya Ulaya, Marekani, Japan  na China  na bei ya katani kutoka dola za Kimarekani 650 kwa tani, mwaka wa 2003/2004 hadi dola 900 kwa tani, mwaka wa 2004/2005. Inatarajiwa kuwa kuongezeka kwa mahitaji ya katani katika soko la kimataifa kutachochea kuongezeka kwa uzalishaji wa katani kwa zaidi ya asilimia kumi kila mwaka.

**Korosho**

**121. Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa korosho unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 22.5, kutoka tani 81,600 zilizozalishwa mwaka wa 2004/2005 hadi kufikia tani 100,000 mwaka wa 2005/2006. Ongezeko hilo linatokana na bei nzuri ya korosho kutoka shilingi 462 kwa kilo, katika msimu wa 2003/2004 hadi shilingi 750 kwa kilo, katika msimu wa 2004/2005  na ruzuku iliyotolewa na Serikali kwa madawa ya maji ya kudhibiti ugonjwa wa ubwiri-unga, ambayo yanatibu ugonjwa huo, badala ya *sulphur* ambayo huzuia tu. Aidha, wakulima wamekuwa na uhakika zaidi wa soko la korosho kutokana na viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa mwaka wa 2004/2005 kuanza kubangua korosho kwa wingi.

**Pamba**

**122. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006 eneo linalotarajiwa kulimwa pamba litaongezeka kutoka hekta 458,836 za msimu wa 2004/2005 hadi hekta 521,422. Aidha, uzalishaji wa pamba unategemewa kuongezeka kutoka tani 344,207 za msimu wa 2004/2005 hadi tani 351,000 mwaka wa 2005/2006. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 2.8, ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka wa 2004/2005. Ongezeko dogo hilo litatokana na hali ya ukame uliyoyakabili

maeneo mengi yanayozalisha pamba kwa wingi nchini kati ya mwezi Februari na Machi, 2005. Katika mwaka wa 2005/2006 Wizara, kupitia Bodi ya Pamba, itaendelea kuhimiza uongezaji wa uzalishaji wa pamba yenye ubora wa juu, kwa kuhimiza matumizi ya mbolea na madawa ya kuulia wadudu katika maeneo yanayozalisha zao la pamba, hususan maeneo ya Kanda ya Magharibi *(Western Cotton Growing Area – WCGA).* Aidha, Wizara itaendelea kuhimiza upanuaji wa maeneo yanayolima pamba, hususan katika Kanda ya Mashariki.

**Pareto**

**123. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, uzalishaji wa pareto unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 1,000 mwaka wa 2004/2005 hadi tani 2,500 sawa na ongezeko la asilimia 150. Ongezeko hilo litatokana na kuongezeka kwa mahitaji ya zao la pareto katika soko la dunia, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya sumu zinazotokana na mazao ya mimea. Hali hiyo imesababisha mwekezaji katika kiwanda cha korosho hapa nchini, kuanza upya mazungumzo na wanunuzi wakubwa waliokuwa wameacha kununua pareto ya Tanzania, miaka minne iliyopita. Aidha, uzalishaji wa pareto utaongezeka kutokana na matumaini ya kufanikiwa kwa mazungumzo kati ya Bodi ya Pareto na wawekezaji ya kujenga hapa nchini kiwanda cha kuchuja sumu. Uzalishaji pia utaongezeka kutokana na Serikali kutoa shilingi bilioni 1.48 zilizotumika kununua tani 1,300 za pareto iliyokuwa mikononi mwa wakulima na hivyo kuwarudishia imani ya kuendelea kuzalisha pareto.

**Sukari**

**124. Mheshimiwa Spika**, katika msimu wa 2005/2006 uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 229,617 zilizozalishwa mwaka wa 2004/2005 hadi tani 277,000 sawa na ongezeko la asilimia 21. Ongezeko hilo litatokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji wa miwa katika kiwanda cha sukari cha Kagera, upanuzi wa Kiwanda cha Mtibwa uliofanyika mwaka wa 2004/2005 na ukarabati wa bwela (*boiler)* la TPC lililokuwa limeharibika msimu wa 2004/2005.

**Tumbaku**

**125. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, uzalishaji wa tumbaku unategemewa kuongezeka kutoka tani 51,000 hadi tani 53,000, sawa na ongezeko la asilimia nne. Ongezeko hilo litatokana na mikakati iliyowekwa na Wizara, kupitia Bodi ya Tumbaku, ya kutoa elimu ya kilimo bora cha tumbaku kuhusu uzalishaji, ukaushaji na upangaji wa tumbaku kwa kuzingatia madaraja ya ubora. Aidha, kuendelea kutumia mbegu na mbolea bora ambazo zinapatikana kwa wakati na kwa viwango vinavyohitajika kunakotekelezwa kwa utaratibu wa kilimo cha mikataba, kutaendelea kuongeza tija na uzalishaji wa zao hilo.

## UENDELEZAJI WA MAZAO YANAYOSTAHIMILI UKAME NA MAZAO YASIYO YA ASILI

**Mazao yanayostahimili Ukame**

**126. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kushirikiana na Idara ya Magereza katika kuanzisha mashamba ya kudumu ya kuzalisha vipando bora milioni 4 vya muhogo na kuhamasisha kilimo cha muhogo katika maeneo yenye ukame na yaliyokumbwa na magonjwa ya muhogo, kama vile ugonjwa wa batobato kali ya muhogo (*CMD-UgV*). Mafunzo ya uzalishaji wa vipando, usindikaji na matumizi ya muhogo yataendelea kutolewa kwa wataalamu wa Idara za Magereza na Halmashauri za Wilaya. Magereza ya wilaya yatakayohusika ni ya mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Kigoma, Tabora, Dodoma, Singida, Kilimanjaro na Arusha.

**127.** Wizara pia itaendelea kuzalisha mbegu za mahindi lishe (*quality protein maize- QPM*) kwa kutumia mashamba ya Serikali na kilimo cha mikataba na sekta binafsi. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Idara ya Magereza kustawisha jumla ya ekari 60 na kuzalisha tani 150 za mbegu za mahindi lishe, zenye ubora wa kuazimiwa (*quality declared seeds-QDS*), katika magereza mawili ya wilaya za Kigoma na Kibondo na shamba la Mbegu la Bugaga, ambazo zitasambazwa katika Halmashauri za Wilaya za mkoa wa Kigoma na mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kagera na Mwanza.

**Mazao ya Thamani**

**128. Mheshimiwa Spika,** Wizara itahimiza kilimo cha zao la soya kwa njia ya mkataba katika mikoa ya Kanda za Nyanda za Juu za Kusini na mikoa mingine yenye sifa na uwezo wa kuzalisha zao hilo nchini. Wakulima watahamasishwa kuzalisha tani 500 za mbegu za soya zenye kiwango cha kuazimiwa (*quality declared seeds -QDS*) ili kuwa chanzo cha mbegu kwa wakulima wengine. Aidha, mafunzo ya kilimo na matumizi ya soya yatatolewa kwa wataalam na wakulima ili kukuza soko na matumizi ya soya nchini.

**129. Mheshimiwa Spika**, Wizara itahamasisha uanzishaji wa hekta 20 za miche bora ya migomba kwa kutumia wakulima katika Halmashauri nne za mikoa ya Kanda ya Ziwa, kama sehemu mojawapo ya juhudi za Serikali za kuendeleza ukanda wa kijani kuzunguka Ziwa Viktoria. Katika mpango huo, machipukizi 154,000 ya migomba yaliyozalishwa kwa chupa (*tissue culture*), yatasambazwa katika wilaya nne za mikoa ya Mwanza na Mara.

**130.** Mkazo utawekwa katika kuhamasisha na kuwezesha wakulima kuanzisha hekta 25 za uzalishaji wa vikonyo na miche bora ya miembe katika mikoa ya Morogoro, Pwani na Dodoma. Mashamba hayo yatakuwa vyanzo vya vikonyo vya miembe bora katika mikoa hiyo. Wizara pia itaendelea kueneza teknolojia ya kilimo cha vanilla katika maeneo mengine nchini kwa kuanzisha ekari 20 za mashamba ya kudumu ya uzalishaji wa vipando vya vanilla katika Halmashauri za Wilaya za Morogoro vijijni na Muheza.

**131. Mheshimiwa Spika**, kazi ya kuendeleza na kuimarisha bustani za vipando vya mazao ya matunda itaendelea kwa kuagiza aina nne bora za mazao ya matunda ya aina ya michungwa, miparachichi, matofaa (*apples*) na mananasi bora kutoka Kenya na Afrika ya Kusini, kwa ajili ya kuizalisha na kuisambaza kwa wakulima. Aidha, jumla ya miche 400,000 ya matunda na viungo inatarajiwa kuzalishwa katika bustani za Jaegetal, Bugaga, Mpiji, Igurusi, Songa na Malindi.

**132.** Wizara itaimarisha uwezo wake wa kutoa elimu ya mbinu za uzalishaji bora

wa mazao mapya yenye thamani na soko la uhakika, wakati wa maonyesho ya Nane Nane.

## HUDUMA ZA UGANI

**133. Mheshimiwa Spika**, utoaji wa huduma za ugani ni muhimu katika kuwafikishia wakulima teknolojia na mbinu mpya za kuendeleza kilimo kwa wakati na kusimamia utekelezaji wa sera na sheria katika ngazi za wilaya na vijiji. Katika miaka ya hivi karibuni, hususan baada ya Serikali kuamua usimamizi na usambazaji wa huduma za ugani ufanyike katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, huduma hizo zimekuwa hazitolewi ipasavyo kutokana na mapungufu katika usimamizi. Katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaagalia upya makubaliano maalum kati yake na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Halmshauri za Wilaya, ili kuiwezesha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuweka utaratibu wa kusimamia utoaji wa huduma za ugani katika ngazi ya wilaya na vijiji. Makubaliano hayo yataainisha utaratibu utakaohakikisha kwamba juhudi za Serikali, hususan, za kuendeleza kilimo chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, hazikwamishwi kutokana na ukosefu wa usimamizi katika ngazi ya utekelezaji. Aidha, kwa utaratibu huo Wizara za kisekta zitatambua matatizo na mahitaji ya wakulima ya teknolojia mpya za kilimo na mbinu za usimamizi na kutoa maelekezo na uwezeshaji wa kuyatatua. Katika kufanikisha lengo hilo, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

- Kufanya uchambuzi wa kina wa mfumo uliopo wa utoaji huduma za ugani na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima. Uchunguzi huo utaainisha majukumu ya wahusika mbalimbali na kupendekeza mfumo na utaratibu unaofaa wa uwajibikaji, utakaosimamia utekelezaji wa majukumu ya wahusika mbalimbali katika utoaji huduma za ugani na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima;

- Kuendelea kuhimiza dhana ya Mbinu Shirikishi Jamii katika kilimo kutoa mafunzo ya dhana hiyo kwa vikundi 300 vya wakulima katika wilaya 25 za mikoa ya Dodoma, Tabora, Morogoro na Pwani. Mashamba darasa 300

yatakayowahusisha wakulima 7,500 yataanzishwa na kuhudumiwa katika wilaya hizo. Aidha, wakulima 200 watapata mafunzo ya kilimo bora katika vyuo vya wakulima vya Bihawana, Dodoma; Ichenga, Njombe; Inyala, Mbeya na Mkindo, Morogoro.

- Kuimarisha kitengo cha Ukulima wa Kisasa makao makuu na kwenye kanda kwa kununua vifaa vya kazi kama kompyuta, kamera za video, mashine za kurekodia sauti na runinga. Vifaa hivi vitakiwezesha kitengo cha Ukulima wa Kisasa kutekeleza majukumu ya kuandaa na kutangaza vipindi vya kilimo redioni na kuchapisha na kusambaza kwa wakulima majarida, vipeperushi, mabango na vijitabu mbalimbali vya kilimo, ikiwa ni pamoja na gazeti la Ukulima wa Kisasa.

## UTAFITI WA KILIMO

**134. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kufanya utafiti ili kuwahakikishia wakulima upatikanaji wa teknolojia bora za kilimo. Juhudi za kuzalisha mbegu bora za mazao ya kilimo zitaendelea. Mkazo utatiliwa katika uzalishaji wa mbegu mpya zitakazomwezesha mkulima kuongeza tija na uzalishaji. Wizara, kupitia vituo vya utafiti, inatarajia kutoa mbegu mpya tatu za jamii ya mafuta, mbegu moja ya jamii ya mikunde na moja ya mpunga. Mbegu hizo zinategemewa kuwa na sifa za mavuno mengi, kustahimili magonjwa na kuvumilia hali ya ukame. Aidha, ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa mbegu za msingi, vituo vya utafiti vitazalisha tani 30 za mahindi, tani 80 za maharage, tani 17 za mpunga, tani mbili za ufuta, tani moja ya karanga na tani 2.6 za kunde. Wizara pia itazalisha mbegu mama za jamii ya nafaka, mafuta na mikunde ambazo ni pamoja na tani 11.3 za mbegu ya mpunga, tani 0.55 za mahindi, tani 0.66 za mtama, tani 0.07 za ufuta, tani 0.2 za karanga na tani 4.36 za mbaazi.

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 Wizara, kupitia vituo vyake vya utafiti, itaendelea na kazi za utafiti wa mazao na mimea ya kilimo zifuatazo:-

- Kutathmini aina tano za mbegu ya nafaka, aina tano za mbegu ya jamii ya mikunde na aina tatu za mbegu za mafuta zenye sifa za kuzaa sana, kustahamili ukame, magonjwa na visumbufu vya mimea;
- Kuzalisha kwa wingi vipando bora vya aina tatu za mazao ya jamii ya mizizi na aina nne za mazao ya biashara katika kanda zote saba za utafiti. Shughuli hizo zitafanyika katika vituo vya utafiti vya Kibaha na Ukiriguru kwa mazao ya muhogo, viazi vitamu na pamba; Uyole, kwa mazao ya viazi mviringo na pareto; Naliendele, muhogo na korosho; Mlingano, mkonge na Ilonga, pamba;
- Kufanya maonesho ya usindikaji na matumizi ya mazao ya jamii ya mizizi, mikunde na mbegu za mafuta katika vijiji vilivyopendekezwa. Usindikaji huo utafanyika katika vituo vya utafiti vya Naliendele, Kibaha na Ukiriguru, mazao ya muhogo; Ilonga, mazao ya mbaazi; Uyole, mazao ya soya na Makutopora, alizeti;
- Kuzalisha na kutunza mbegu mama za mazao ya jamii ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta;
- Kuendeleza utafiti wa mazao matano ya viungo, mazao matano ya mboga na mazao matano ya matunda katika vituo vya utafiti na katika mashamba ya wakulima;
- Kuendeleza na kuimarisha shughuli za Kitengo cha Hifadhi ya Nasaba za mimea (NPGRC);
- Kubuni, kutathmini na kusambaza mbinu tano bora na endelevu za kuzalisha mazao ya jamii za nafaka, mikunde, ndizi, minazi na zabibu katika kanda saba za utafiti wa kilimo.

Ufafanuzi wa kina wa kazi za utafiti zitakazotekelezwa umeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 10

**136. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, Wizara itaendelea kutafiti mbinu za kuongeza virutubisho katika mashamba. Wizara, ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, itatafiti mbinu mbali mbali za uvunaji maji ya mvua (*rain water harvesting*) ili kuboresha uzalishaji wa mazao katika maeneo yenye uhaba wa mvua. Aidha, Wizara kupitia vituo vya Tumbi, Selian, Uyole na Ukiriguru, itaendelea kufanya utafiti wa miti inayoweza

kutumiwa katika kilimo mseto. Wizara pia itaendeleza utafiti wa matumizi ya wanyamakazi na zana mbalimbali za kilimo katika kutayarisha mashamba, kupanda, kupalilia na kubeba mizigo. Utafiti huo utawashirikisha wakulima katika mashamba yao.

**137. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kuwashirikisha wakulima katika shughuli za utafiti, hususan katika kuwafundisha watafiti mbinu bora za utafiti shirikishi. Mbinu hizo zitawezesha watafiti kuchambua matatizo ya wakulima kwa kuhusisha wakulima wenyewe. Watafiti 40 watapata mafunzo hayo. Aidha, utafiti mbalimbali wa sayansi jamii na uchumi kuhusiana na usambazaji wa teknolojia mpya miongoni mwa wakulima na matokeo yake zitaendelea kutekelezwa kwenye Kanda mbalimbali za utafiti. Wizara itaandaa na kuratibu mikutano itakayohusisha wakulima, watafiti na wadau mbalimbali wa utafiti katika kanda zote saba za utafiti.

**138. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaweka utaratibu wa kutangaza matokeo ya utafiti na kuzawadia watafiti waliohusika. Aidha, utaratibu wa kuwazawadia watafiti watakaogundua aina mpya za mbegu na teknolojia mbalimbali utaendelea, ikiwa ni pamoja na kuwapatia sehemu ya mapato yatakayotokana na haki miliki baada ya ugunduzi huo kusajiliwa, chini ya sheria ya Haki Miliki za Wazalishaji wa Mbegu na Mimea Mipya ya mwaka 2002.

**139.** Wizara pia itaandaa takwimu za mafanikio ya teknolojia zilizopelekwa kwa wakulima na itaimarisha mfumo wa habari kwa menejimenti ya utafiti ili kufanikisha maandalizi ya mipango bora ya utafiti inayolenga kutatua matatizo ya wakulima. Kanda zote saba za utafiti zitaandaa maonyesho ya teknolojia mbalimbali zilizofanyiwa utafiti, yatakayofanyika katika vituo vya utafiti na viwanja vya maonyesho ya Nane Nane. Wakulima na wadau wengine watahamasishwa kwenda kuangalia maonyesho hayo. Wizara pia itaendelea kuboresha huduma za utoaji habari za utafiti kwa wadau, kupitia machapisho na mtandao wa *internet.*

**140. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, watafiti na watumishi wengine wanaojishughulisha na kazi za utafiti wapatao 100 watapata mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

## KILIMO CHA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI

**141. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula itakuwa inatekeleza mwaka wa nne wa Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Mpango huo umeainisha hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Mpango huo unoanyesha kuwa ili mazao yatokanayo na kilimo cha umwagiliaji maji mashambani yatosheleze Taifa kwa chakula, hususan zao la mpunga ifikapo mwaka wa 2017, eneo la hekta 405,400 litapaswa liendelezwe kwa kilimo hicho. Ili lengo hilo lifikiwe, tutapaswa kuendeleza sio chini ya hekta 30,000 kila mwaka. Ili kufikia lengo hilo, Serikali inapaswa kuwekeza zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa mwaka.



**142. Mheshimiwa Spika**, kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachohitajika kutekeleza Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani,

ni dhahiri kwamba fedha za bajeti ya Serikali peke yake hazitoshi. Hivyo, ipo haja ya Serikali kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kuweka mazingira ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika kuendeleza kilimo hicho. Kama sehemu ya utekelezaji wa lengo hilo, Wizara itaandaa utaratibu madhubuti unaosimamiwa na sheria, utakaohakikisha uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji mashambani unafuata taratibu na kanuni za kitaalam. Aidha, zitahakikisha ardhi iliyoendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani inatumiwa kwa njia endelevu. Katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itapeleka mapendekezo serikalini ya kutungwa kwa Sheria ya Umwagiliaji Maji Mashambani, itakayopendekeza, pamoja na mambo mengine, kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani na kuweka utaratibu wa kisheria wa matumizi bora na endelevu ya ardhi inayoendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

**143. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula itaweka mfumo bora wa matumizi ya takwimu zilizotayarishwa chini ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Kazi hiyo itahusisha pia ukusanyaji wa takwimu za miradi ya umwagiliaji maji mashambani inayogharamiwa na kuendeshwa na wadau mbalimbali na kuielekeza katika utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Aidha, Wizara itatayarisha mwongozo wa kitaalamu ambao utatumika katika kutathmini gharama za utayarishaji wa miradi ya umwagiliaji maji mashambani itakayotekelezwa chini ya DADPs.

**144. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara imelenga kuongeza eneo la uzalishaji kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kwa hekta 19,542. Kati ya hizo, ujenzi wa hekta 14,521 utakamilishwa mwaka wa 2005/2006 na ujenzi wa hekta 5,021 utakamilishwa mwaka 2006/2007. Ongezeko hilo, litafanya jumla ya eneo la kilimo cha umwagiliaji maji mashambani nchini kufikia hekta 264,513 kutoka hekta 249,992 zilizokuwa zimeendelezwa hadi mwaka wa 2004/2005.

**Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani na Ujenzi wa Mabwawa**

**145. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendeleza skimu 92 zenye jumla ya hekta 18,912 kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani. Mashamba ya Serikali ya Mbegu ya Dabaga, Kilolo na Arusha, Arumeru yatajengewa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani. Aidha, mabwawa yenye uwezo wa kumwagilia hekta 1,700 yatajengwa katika wilaya za Iramba, Musoma, Serengeti, Nzega, Urambo, Uyui, , Kilosa, Bagamoyo na Muheza (Kiambatisho Na 11).

**Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani**
***(Participatory Irrigation Development Programme – PIDP)***

**146. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika maeneo ya ukame katika skimu 12 zenye eneo la hekta 2,498, ambazo ujenzi wake uko kwenye hatua mbalimbali. Aidha, programu hii itaanza ujenzi wa miundo mbinu ya umwagiliaji maji mashambani katika skimu 10 nyingine zenye ukubwa wa hekta 2,871.

**Miradi ya Umwagiliaji Maji Mashambani chini ya Mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo (*District Agricultural Development Plans – DADPs*)**

**147. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendeleza miradi 30 yenye eneo la hekta 5,000 ambayo itakuwa imeibuliwa na kuwekwa kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani chini ya Programu ya**

**Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASPS II)**

**148. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2005, Wizara itaendelea kujenga skimu ya umwagiliaji maji mashambani ya Naming'ongo wilayani Mbozi yenye ukubwa wa hekta 1,000. Ujenzi wa skimu hiyo utakamilika mwezi wa Disemba, 2005.

**Skimu zilizogharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula (*Food Aid Counterpart Fund*).**

**149. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itakarabati skimu saba zenye jumla ya hekta 1,350 zitakazogharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula *(Food Aid Counterpart Fund).* Skimu hizo ziko katika wilaya za Tarime, Hai, Bukoba, Namtumbo, Iringa Vijijini, Karagwe (Kagenyi), Kibondo na Mvomero.

**Skimu za Mfano za Umwagiliaji Maji Mashambani katika Mwambao wa Ziwa Viktoria na Ziwa Nyasa**

**150. Mheshimiwa Spika,** mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kuendeleza skimu za mfano katika ukanda wa Ziwa Viktoria, kwa lengo la kuwahamasisha wakulima kuiga kutumia maji ya Ziwa kwa teknolojia ya kuvuta maji kwa kutumia pampu zinazotumia nguvu ya upepo, mafuta ya dizeli, mionzi ya jua na pampu za kusukuma kwa miguu. Hekta 100 zitaendelezwa katika mwambao wa Ziwa Viktoria. Aidha eneo lingine la hekta 100 zitaendelezwa kwa maksudi na utaratibu huo huo katika mwambao wa Ziwa Nyasa.

**151. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendelea kusimamia skimu zote za umwagiliaji maji mashambani ili kuhakikisha kwamba malengo ya tija na uzalishaji yaliyowekwa katika skimu hizo yanafikiwa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wakulima yanayohusu matumizi bora ya maji na uendeshaji na usimamizi wa skimu za umwagiliaji maji mashambani.

## MAFUNZO YA KILIMO KWA WATAALAM NA WAKULIMA

**152. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wataalam wa Wizara, maofisa wa ugani wa wilaya na wakulima, ili kuhakikisha kuwa Programu ya Kuendeleza Kilimo inatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya ubora na taaluma za kisasa. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na:-

**Mafunzo kwa wakulima**

- Kufundisha Kilimo bora cha mazao na mbinu za kuongeza ubora wa mazao hayo;
- Kuandaa vitini vya "*modules*" za mazao mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya wakulima;
- Kufundisha matumizi ya mboji ili kupunguza matumizi ya kemikali katika Kilimo;
- Kufundisha matumizi bora ya wanyamakazi katika vyuo vinane vya Kilimo;
- Kufundisha matumizi ya majiko sanifu yenye kutumia nishati ndogo ili kupunguza ukataji holela wa miti kwa ajili ya nishati.

**Mafunzo kwa Maafisa Ugani**

- Kutoa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Stashahada kwa maafisa ugani 200 wa mwaka wa kwanza na maafisa 250 mwaka wa pili;
- Kuandaa vitini vya kufundishia mazao mbalimbali, hususan mazao ya biashara yanayolimwa nchini na pia yale yenye thamani kubwa;
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi yanayohusu matumizi bora ya ardhi na maji ili kupunguza uharibifu wa ardhi na kuongeza uzalishaji wa mazao.

**Mafunzo kwa Wataalam**

- Kugharamia mafunzo katika ya ngazi ya shahada ya uzamili kwa wakufunzi sita na mafunzo katika ngazi ya shahada ya udaktari wa falsafa

kwa mkufunzi mmoja;

- Kugharamia mafunzo ya muda mfupi ya mbinu za kufundishia kwa waalimu 50 ili kuinua viwango na mbinu za kutoa elimu.

**Usimamizi na huduma**

- Uchapishaji wa nakala za vitabu rejea vitakavyouzwa kwa bei nafuu kwa wagani na wanachuo;

- Kulipia ada vyuo saba ili viweze kupata usajili wa Baraza la Mitihani la Taifa (*The National Council for Technical Education* - *NACTE*);

- Kusimamia bodi za mitihani na kuhakiki utungaji wa mitihani na kuhakiki matokeo kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa;

- Kuandaa mkutano mkuu wa mwaka wa wadau wa kilimo na mifugo ili kutathmini utoaji wa taaluma vyuoni na jinsi ya kuuimarisha.

## MATUMIZI YA PEMBEJEO NA ZANA ZA KILIMO

**153. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006 Wizara itaendelea kuweka vivutio vitakavyochochea kupanuka kwa soko la ndani na matumizi ya pembejeo za kilimo.

**Mbolea na Madawa**

**154. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006 inatarajiwa kuwa upatikanaji wa mbolea utaongezeka kutoka tani 195,065 zilizopatikana mwaka wa 2004/2005 hadi tani 385,000. Ongezeko hilo litatokana na uwekezaji unaotarajiwa kutoka makampuni ya biashara ya mbolea ya kimataifa. Makampuni hayo ni YARA kutoka Norway na SSE kutoka Afrika ya Kusini, ambayo yanatarajiwa kufungua maghala makubwa ya kuhifadhia na kuuzia mbolea nchini. Inatarajiwa kwamba uhakika wa upatikanaji wa mbolea utachangia kuongezeka kwa matumizi ya mbolea nchini. Lengo ni kufikia wastani wa kilo kumi kwa hekta ifikapo mwaka wa 2007/2008. Wizara pia imepanga kuongeza matumizi ya madawa ya korosho kutoka lita 3,000 hadi lita 10,000 ifikapo

mwaka wa 2007/2008.

**Ruzuku ya Mbolea**

**155. Mheshimiwa Spika,** kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea miaka miwili iliyopita, mwaka wa 2005/2006 Serikali itaendelea kufidia usafirishaji wa mbolea kwa nchi nzima na madawa ya korosho katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Tanga, Morogoro na Dar-es-salaam. Tani 75,000 za mbolea na lita 5,000 za madawa ya korosho zinatarajiwa kuhusika katika utaratibu huo. Shillingi bilioni 1.0 zitahitajika kufidia sehemu ya gharama za madawa ya korosho na shilingi bilioni 7.50 zitatumika kufidia gharama za usafirishaji wa mbolea.

**156. Mheshimiwa Spika,** uzoefu wa miaka miwili iliyopita wa utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea, unaonyesha kwamba kuna mapungufu ya usimamizi, hususan katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Usimamizi wa mpango wa ruzuku wa Kamati za mikoa na wilaya unahitajika sana, kuhakikisha mbolea zenye ruzuku zinazosafirishwa hadi vituo vikuu vya usambazaji vya mikoa, zinasafirishwa hadi wilayani na baadaye kwenye maduka, ambapo wakulima wataweza kuzinunua kwa bei zilizopangwa. Kamati hizo zina wajibu na haki ya kuingilia kati mara inapogundulika kwamba utaratibu wa ruzuku unakiukwa.

**157.** Ili kuondoa mapungufu katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea yaliyojitokeza katika miaka iliyopita, katika mwaka wa 2005/2006 Wizara itaendesha mikutano ya kuhamasisha Makatibu Tawala wa Mikoa 21, Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya 114 na Washauri wa Kilimo wa Mikoa 21, juu ya utaratibu wa kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea na madawa ya korosho. Aidha, mikutano hiyo itawezesha watekelezaji hao kuelewa wajibu na majukumu yao na kukubaliana juu ya utaratibu wa aina moja wa kuyatekeleza. Aidha, Wizara itagharamia mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za pembejeo za kilimo kwa watakwimu 60 kutoka wilaya na mikoa ya Kigoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Lindi na Mtwara.

**Mbegu Bora**

**158. Mheshimiwa Spika,** makisio ya mahitaji ya mbegu zilizothibitishwa katika msimu wa 2005/2006 ni tani 30,000. Upatikanaji wa mbegu, unatarajiwa kuwa jumla ya tani 13,800 ambazo zitatokana na uzalishaji katika makampuni binafsi ya hapa nchini, tani 3,800; mbegu zitakazozalishwa na wakulima wadogo, tani 700; mbegu kutoka nje ya nchi, tani 7,800 na uzalishaji katika mashamba ya Serikali, tani 1,500. Jumla ya hekta 1,000 za mashamba ya mbegu ya Serikali ya Msimba, hekta 200; Arusha, hekta 328; Mwele, hekta 110; Kilangali, hekta 140; Dabaga, hekta 220 na HORTI Tengeru, hekta 2, zitahusika katika kuzalisha mbegu hizo.

**159. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha udhibiti wa ubora wa mbegu, mafunzo ya ukaguzi wa mbegu yatatolewa kwa maafisa ugani 50 kutoka wilaya 50 za Tanzania Bara. Aidha, Wizara, itaendelea kuratibu mpango wa uzalishaji wa mbegu kwa wakulima wadogo vijijini katika wilaya 6 za mikoa ya Kigoma na Pwani. Wakulima hao watafundishwa jinsi ya kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa kwa mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta.

**Zana za Kilimo**

**160. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kuhimiza matumizi ya zana bora. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, itakayowawezesha kukarabati matrekta mabovu, kununua matrekta mapya na zana zinazokokotwa na wanyamakazi. Jumla ya matrekta 114 yatakarabatiwa na matrekta makubwa mapya 28 yatanunuliwa chini ya mpango huu.

**161. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itakamilisha ukarabati wa vituo vya maksai 30. Vituo hivyo ni Lyangu, wilayani Njombe; Masonya, Tunduru; Mifipro, Mwanga; Konje, Handeni; Pimbi, Kyela; Ngimu, Singida Vijijini; Kabungu, Mpanda; Katumba, Sumbawanga Mjini; FDC, Sikonge, Katesh, Hanang; Gairo, Kilosa; Korogwe; Rujewa, Mbarali; Chikola, Manyoni; Mwese, Mpanda; Kate, Nkasi; Msangano, Mbozi; Mapogoro, Ileje; Inonelwa, Misungwi; Kipalapala, Tabora; Lilambo, Songea; Malagarasi, Kigoma;

Chamkoroma, Kongwa; Burunga, Serengeti; Buhemba, Musoma; Kitowo, Iringa; Kishinda, Sengerema; Kibakwe, Mpwapwa; Kisangwa, Bunda na Bangayega, Manyoni. Aidha, vituo hivyo vitapatiwa zana bora kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima.

**162. Mheshimiwa Spika,** ili kusambaza elimu ya matumizi ya zana bora za wanyamakazi, Maafisa Ugani 300 kutoka wilaya 30 watapata mafunzo. Maafisa ugani hao watatoa mafunzo kwa vitendo kwa wakulima katika vikundi ili kusambaza teknolojia hiyo kwa wakulima wengi zaidi. Vikundi 100 vyenye wakulima kati ya 10 na 20 wa kilimo cha maksai vitaanzishwa na vitafundishwa matumizi ya zana kwa vitendo, chini ya usimamizi wa Maafisa Ugani.

**163. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, msukumo utawekwa katika kuendeleza zana za kilimo hifadhi ili kuendeleza kilimo chenye tija kwa kutumia zana zinazopunguza uharibifu wa ardhi na mazingira. Vikundi vya wakulima 130 vyenye wakulima 3,250 vitaanzishwa na kupewa mafunzo ya zana za kilimo hifadhi katika wilaya 13 za Morogoro, Kilosa, Mbeya Vijijini, Ileje, Mbarali, Mufindi, Njombe, Iringa, Singida Mjini na Vijijini, Babati, Hanang na Muheza. Katika kutoa mafunzo hayo mashamba ya mfano 886 yataanzishwa ili kuwawezesha wakulima kujifunza teknolojia hiyo kwa vitendo**.**

**164. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006 Wizara itatoa mafunzo juu ya matumizi, utengenezaji na utunzaji wa matrekta makubwa na madogo ya mkono kwa maafisa zana 50 na waendesha matrekta 20. Maafisa zana hao watatoa ushauri wa kiufundi kwa wakulima wenye matrekta hayo vijijini. Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya uendeshaji wa mashine ndogo za kubangua korosho, kusindika muhogo na kukamua alizeti kwa maafisa ugani 40, ambao wataendelea kutoa mafunzo kwa vikundi vya wakulima. Ili kuendeleza matumizi ya teknolojia rahisi, hususan kwa wanawake, Wizara, kwa kushirikiana na taasisi ya *CAMARTEC*, itatoa mafunzo kwa vikundi 50 vya kinamama kutoka Halmashauri za wilaya 15 kuhusu matumizi ya majiko sanifu na nishati mbadala za ukaushaji wa mazao.

**Mfuko wa Pembejeo**

**165. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Pembejeo utaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya kununulia pembejeo na zana za kilimo, kupitia mabenki na Shirikisho la Vyama vya Kuweka na Kukopa Tanzania (SCULT). Mikopo hiyo itatolewa kwa masharti ya ukopeshaji ya kibenki. Aidha, Mfuko utaendelea kuboresha utaratibu na mtandao wa usambazaji wa pembejeo, ili kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo na zana kwa wakati na kwa bei nafuu. Mfuko pia utaendelea kukusanya madeni ya miaka ya nyuma, ikiwa ni pamoja na uuzaji wa dhamana za wadaiwa.

## MATUMIZI BORA YA ARDHI

**166. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kuweka msukumo mkubwa katika kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ili kukukifanya kilimo kuwa endelevu na kisichoharibu mazingira. Wizara itaelekeza nguvu zake katika kazi zifuatazo:-

- Kuhifadhi vyanzo vya maji vya skimu za umwagiliaji maji mashambani za Madibira, Mbarali; Lumuma, Kilosa na Kikafuchini, Hai ili kudhibiti mmomonyoko wa udongo mashambani.
- Kupima mashamba katika maeneo ya kilimo kwenye wilaya za Singida, Songea na Morogoro vijijini.
- Kupanua maeneo ya mfano wa kudhibiti mmomonyoko wa udongo mashambani katika wilaya 36 za mikoa ya Dododma, Singida, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Mwanza, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Iringa na Ruvuma.
- Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani kutoka wilaya 80 juu ya hifadhi ya udongo namatumizi bora ardhi ili waweze kuwaelimisha wakulima walioko kwenye maeneo yao ya kazi.

## UDHIBITI WA VISUMBUFU VYA MIMEA NA MAZAO YA KILIMO

**167. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na

Chakula itaendelea kuhamasisha wakulima wa mikoa ya Kigoma, Singida, Mtwara, Lindi, Morogoro, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na mikoa ya kanda ya ziwa kuanzisha na kuendeleza matumizi ya mbinu ya udhibiti husishi wa visumbufu vya mimea kama njia pekee endelevu na salama ya kudhibiti visumbufu hivyo. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Mashirika ya Kimataifa yanayodhibiti milipuko ya nzige na *Quelea quelea*, kukagua maeneo ya mazalio ya visumbufu hao na kuwadhibiti mapema ili kuokoa mazao ya wakulima. Utabiri wa milipuko kwa baadhi ya visumbufu kama viwavijeshi na panya utaimarishwa. Aidha, uchunguzi na udhibiti wa gugumaji utaendelezwa. Katika juhudi za kupambana na inzi wa matunda aliyebainika kuenea sehemu kubwa ya nchi, mikakati mbalimbali, ikiwa ni pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wakulima kuhusu njia za kumdhibiti mdudu huyo itatekelezwa.

## HIFADHI YA MAZAO NA USALAMA WA CHAKULA

**168. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa 2005/2006 Hifadhi ya Taifa ya Chakula inatarajia kununua jumla ya tani 39,000 za mahindi na hivyo kuwezesha Kitengo kuwa na hifadhi ya tani 152,000. Gharama za ununuzi wa tani 39,000 za mahindi zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 5. 850. Kitengo kitahitaji pia vitendea kazi kama magunia, maturubai, mizani na madawa vinavyokadiriwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 2.25. Uhamishaji wa hifadhi ndani ya Kanda unakadiriwa kugharimu shilingi milioni 270. Aidha, gharama za uendeshaji wa ofisi za Kanda na Makao Makuu zinakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi 426, 497,500.

### Hifadhi ya Chakula katika ngazi ya Taifa

**169. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo na Chakula ina jukumu la kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa chakula kwa wakati wote. Ili kufikia lengo hilo, katika mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuboresha mfumo wa ukusanyaji takwimu na taarifa za chakula nchini;

- Kukusanya taarifa za mvua na mazao na kufanya tathmini ya kaya zilizoathirika na upungufu wa chakula;

- Kuendesha kampeni ya ukadiriaji na hifadhi ya chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya kwa mikoa 11 ya Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Pwani, Kagera, Kigoma, Mtwara, Lindi na Tanga;

- Kutoa mafunzo ya kusambaza teknolojia za hifadhi, usindikaji na elimu ya lishe kwa mazao ya mtama, mizizi, mboga na matunda katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Manyara, Mwanza, Mara, Shinyanga na Kilimanjaro.

## UBINAFSISHAJI WA MASHAMBA NA MASHIRIKA YA KILIMO

**170. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) kubinafsisha mali za mashirika na mashamba ambayo bado hayajabinafsishwa. Mashirika na mashamba hayo ni pamoja na mashamba ya kahawa yaliyoko Mbozi, mashamba ya mahindi ya Mbozi na Namtumbo na mashamba ya mpunga ya Mbarali na Kapunga. Aidha, shamba la chai na kiwanda cha chai cha Dabaga na mali za NMC zilizoko Mwanza zitabinafsishwa upya baada ya kurudishwa Serikalini, kutokana na wawekezaji kushindwa kutimiza masharti ya mikataba ya ubinafsishaji.

**171. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya mauzo ya mashirika yaliyobinafsishwa ili kuhakikisha kuwa malengo ya ubinafsishaji wa mali hizo yanafikiwa. Maeneo yatakayofuatiliwa ni pamoja na viwanda vya Sukari, vinu vya NMC, kampuni ya kuchambua pamba ya Manawa, mashamba ya mkonge, mashamba yaliyokuwa yanamilikiwa na NAFCO na mashamba na kiwanda cha pareto cha Iringa.

## KUREKEBISHA NA KUHUISHA SHERIA

**172. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara itaendelea

kusimamia Sheria na Kanuni za sekta ya kilimo ili kuhakikisha malengo yaliyosababisha kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa. Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni muswada wa kutunga Sheria ya Kulinda na Kuendeleza Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula (*Plant Genetic Resources for Food and Agriculture*) ili kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Nasaba za Mimea kwa Ajili ya Kilimo na Chakula wa mwaka 2001, ulioridhiwa na Serikali ya Tanzania mwaka wa 2003. Aidha, utaratibu wa kupata kibali cha Serikali cha kuleta muswada wa sheria ya Mbolea Bungeni, utakamilishwa. Serikali pia itarekebisha sheria ya Udhibiti wa Viumbe Waharibifu wa Mimea na Mazao, ya mwaka wa 1997 (*The Plant Protection Act, 1997*) ili itumike kutekeleza Mikataba ya Kimataifa ambayo Serikali imeridhia, ikiwa ni pamoja Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao, wa mwaka wa 1952 (*The International Plant Protection Convention, 1952*). Sheria iliyoanzisha Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu ya mwaka wa 1989 (*The Tropical Pesticide Act, 198*9) na sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka 1991 (*The Food Security Act, 1991*) nazo pia zitafanyiwa marekebisho ili zikidhi mahitaji ya wakati uliopo.

**173. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa 2005/2006 Wizara itakamilisha uchunguzi wenye lengo la kutunga sheria ya kusimamia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani, ili kuweka utaratibu wa matumizi endelevu ya ardhi inayotumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Wizara pia itafanya uchunguzi wenye lengo la kutunga sheria ya kulinda ardhi inayotumika kwa ajili ya kilimo, ili itumiwe kwa njia endelevu, ichochee uzalishaji wenye tija na kuweka usimamizi wa kilimo cha kisasa na cha kibiashara. Aidha, uwezekano wa kuwa na sheria maalum ya kusimamia taasisi za utafiti wa kilimo utachunguzwa.

## MAENDELEO YA WATUMISHI

**174. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ya Kilimo na Chakula itawaendeleza watumishi wake kielimu na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi, yatakayowawezesha kutekeleza kwa ufanisi Mpango wa Maendeleo ya kilimo wa mwaka 2005/2006. Mkazo utawekwa katika mambo muhimu yafuatayo:-

- Kutoa mafunzo kwa watumishi ili kukidhi mahitaji ya miundo mipya ya utumishi (*Scheme of Service*) na kuimarisha uwezo wao wa utendaji. Mafunzo yatatolewa pia kuhusu sheria mpya za kazi, kanuni na taratibu za uendeshaji kazi Serikalini uzingatiaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Namba 8 ya mwaka wa 2002 na Mpango wa Uboreshaji kazi Serikalini (*PSRP*);

- Kupandisha vyeo watumishi kulingana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma.;

- Kuajiri watumishi wapya 131 ili kuboresha utendaji kazi katika Idara na Vitengo mbalimbali;

- Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi ya watumishi kwa kuwawekea watumishi hao vitendea kazi bora kwa kuzingatia bajeti na malengo yaliyowekwa;

- Kukusanya na kukagua taarifa za watumishi (*Human Resources Audit*) wa Wizara ili kukamilisha kazi ya kuweka kwenye kompyuta kumbukumbu sahihi za watumishi;

- Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu matumizi ya fomu ya wazi ya mapitio na upimaji utendaji kazi wa wafanyakazi *(OPRAS*), ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa mteja *(Client Service Charter*);

- Kuhamasisha watumishi kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Rushwa (*NASCAP*). Aidha, Wizara itahamasisha watumishi waliopo vituoni wawajibike ipasavyo kulingana na maadili ya utendaji katika maeneo yao ya kazi;

- Baada ya kupitia upya mpango mkakati wa UKIMWI (*Strategic Plan for HIV/AIDS, 2005/06-2007/08*) Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa

watumishi waliopo vituoni kuhusu lishe bora kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na jinsi ya kujikinga na maambukizo mapya ya virusi vya UKIMWI.

## HITIMISHO

**175. Mheshimiwa Spika**, napenda kuhimitisha hotuba yangu kwa kuwashukuru sana Waheshimia Wabunge wote kwa ushauri na michango yenu mliyokuwa mkitoa kwa Wizara ambayo tumekuwa tukiizingatia katika utekelezaji wa Mipango ya Kuendeleza sekta ya Kilimo. Ushauri na michango hiyo, ililenga katika kukiendeleza kilimo kwa nia ya kukifanya kiwe cha kisasa, chenye tija na kitakachotoa mchango mkubwa zaidi katika Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini. Matokeo ya utekelezaji wa mipango ya kuendeleza kilimo, yameanza kuonekana. Kwa mfano, sekta ndogo ya mazao ilikua kwa asilimia 3.5 mwaka wa 2000 na kwa asilimia 6.2 mwaka wa 2004. Uzoefu katika utekelezaji wa mipango ya kuendeleza kilimo unaonyesha kuwa inawezekana kabisa kukifanya kilimo kikue na kutoa mchango unaostahili katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Lengo hilo linaweza kufikiwa ikiwa kilimo kitakua kwa zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka. Kuna mambo muhimu ambayo yanapaswa yafanyike ili lengo hilo lifikiwe.

**176. Mheshimiwa Spika,** viwango vya matumizi ya mbolea nchini ni vya chini sana ikilinganishwa na viwango vinavyoshauriwa na wataalam. Kwa mfano, wastani wa matumizi ya mbolea nchini ni kilo 7 tu kwa hekta, ikilinganishwa na kilo 60 kwa hekta, zinazopendekezwa. Ili kufikia lengo, ipo haja ya kuweka mikakati itakayohakikisha viwango vya upatikanaji na matumizi ya mbolea vinaongezeka kutoka tani 195,065 zilizopatikana mwaka wa 2004/2005 hadi tani 600,000 kwa mwaka. Kama sehemu ya mkakati wa kufikia lengo hilo, mwaka wa 2005/2006 Serikali, kwa kushirikiana na sekta binafsi na makampuni makubwa ya kimataifa, inatarajia kuongeza upatikanaji wa mbolea kufikia tani 385,000.

**177. Mheshimiwa Spika,** unahitajika umakini wa hali ya juu katika kusimamia rasilimali za uzalishaji na Mipango ya Maendeleo ya Kilimo, kuanzia ngazi ya Taifa,

Wilaya hadi Kijiji. Hivyo, ili kuhakikisha kwamba huduma za ugani zinawafikia wakulima kwa ufanisi zaidi, Halmashauri za Wilaya zitapaswa kuweka utaratibu madhubuti wa kusimamia utendaji kazi wa maofisa ugani na kuhakikisha unatekelezwa.

**178. Mheshimiwa Spika,** juhudi za Serikali za kukifanya kilimo kikue zitakuwa na ufanisi zaidi iwapo kutakuwepo na mkakati wa kuondokana na kilimo cha kujikimu na kuimarisha kilimo cha kibiashara. Ili kufikia lengo hilo, mafunzo yanayotolewa kwa wakulima, mabwana shamba na wataalamu, itabidi yazingatie mahitaji ya msingi ya kilimo cha kibiashara ili yawapatie wakulima utalaamu wa kutathmini mahitaji ya msingi ya kuwawezesha kuendesha kilimo hicho. Mahitaji hayo ni pamoja na ardhi, mitaji ya kununulia pembejeo, gharama za nguvu kazi na upatikanaji wa soko la uhakika. Ili kufikia lengo hilo, kilimo cha kibiashara cha wakulima wakubwa na wakati itabidi kiimarishwe kuwezesha wakulima wadogo wajifunze kutoka kwao.

**179. Mheshimiwa Spika, uendelezaji** wa kilimo cha kibiashara utahitaji nidhamu, hususan katika matumizi ya rasilimali muhimu za uzalishaji, ambazo ni pamoja na ardhi na nguvu kazi. Umiliki wa ardhi kwa ajili ya kilimo cha kibiashara unapaswa uzingatie kiwango cha chini cha ukubwa wa ardhi kitakachomwezesha mkulima kuzalisha kibiashara. Aidha, ugawanyaji wa ardhi katika vishamba vidogo vidogo vya wakulima, unapaswa usitishwe kwa sababu unaifanya ardhi hiyo isifae kwa kilimo cha kibiashara. Utaratibu wa kisheria utakaohakikisha kuwa ardhi bora kwa ajili ya kilimo inalindwa na inagawanywa kwa kuzingatia masharti ya kilimo cha kibiashara, utapaswa kuwekwa.

**180. Mheshimiwa Spika,** kilimo chetu kitakuwa cha kibiashara, iwapo kitaendelezwa kwa kuzingatia masoko ya nje na ya ndani. Kwa takriban miaka minne iliyopita, Serikali imekuwa ikidhamini mauzo ya mazao ya nje ya nchi, kupitia utaratibu wa "*Export Credit Guarantee Scheme*". Pamoja na juhudi hizo, utangazaji wa mazao ya Tanzania kwenye masoko ya nje, hususan mazao yenye thamani na uhakika wa upatikanaji wa soko, yakiwemo mazao ya mboga, matunda na viungo, unapaswa utiliwe mkazo. Aidha, ili mazao yetu yapate soko la uhakika, yatapaswa yazalishwe na kutunzwa kwa ubora wa hali ya juu, utakaoyawezesha kustahimili ushindani katika soko la kimataifa.

**181. Mheshimiwa Spika,** mkakati mmojawapo wa kuyaongezea ubora mazao ya kilimo ni kuimarisha mfumo wa kuongeza thamani kwenye mazao, ili kupunguza uharibifu baada ya kuvunwa na kuyafanya yauzwe kwa bei nzuri zaidi. Kwa

kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, wawekezaji katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo watapaswa wapewe vivutio, ili wawekeze katika viwanda vya kusindika mazao ya kilimo. Hatua hii pia itasaidia kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, hususan vijana na wanawake.

## SHUKRANI

**182. Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani za dhati kwa nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yanaendelea kuisaidia Wizara ya Kilimo na Chakula katika juhudi za kuleta mapinduzi katika sekta ya Kilimo. Nchi hizo ni China, Canada, Denmark, Finland, India, Ireland, Israel, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubeligiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Norway na Sweden. Napenda pia kuyashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kama ifuatavyo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, BADEA, UNDP, FAO, JICA, DFID, EU, UNICEF, WFP, IFAD, CIMMTY, ACRISAT, ASARECA, USAID, GTZ, IITA, DLCO-EA, IRLCO-CSA na *Sasakawa Global 2000*. Bado tunahitaji misaada na ushirikiano wao ili kuendeleza Kilimo nchini.

## MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2005/2006

**183. Mheshimiwa Spika,** naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 118,124,823,900 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa 2005/2006, kati ya fedha hizo, shilingi 54,634,823,900 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara na shilingi 63,490,000,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, shilingi 7,440,000,000 sawa na asilimia 11.7 ni fedha za ndani na shilingi 56,050,000,000 sawa na asilimia 88.3 ni fedha za nje.

**184. MHESHIMIWA SPIKA, NAOMBA KUTOA HOJA**

*Kiambatisho 1*

UZALISHAJI WA MAZAO YA CHAKULA NA KIWANGO CHA UTOSHELEVU KUANZIA MWAKA WA 1994/95 HADI **2004**/**2005** **(TANI)**

| Mwaka | Uzalishaji | Kiwango cha utoshelevu (%) |
|---|---|---|
| 1994/1995 | 7,719,200 | 95 |
| 1995/1996 | 8,020,700 | 110 |
| 1996/1997 | 6,181,400 | 117 |
| 1997/1998 | 8,138,380 | 88 |
| 1998/1999 | 7,440,531 | 109 |
| 1999/2000 | 7,323,000 | 108 |
| 2000/2001 | 7,584,000 | 92 |
| 2001/2002 | 8,572,288 | 94 |
| 2002/2003 | 7,372,720 | 102 |
| 2003/2004 | 9,000,000 | 88 |
| 2004/2005 | 9,790,000 | 103 |
| Jumla | 87,142,219 | |
| Wastani | 8.7 | 100.55 |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula*

*Kiambatisho 2*

MIRADI ILIYOIBULIWA NA KUTEKELEZWA CHINI YA MRADI SHIRIKISHI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UWEZESHAJI (PADEP)

| Wilaya | Kilimo bora cha mazao | Ufugaji bora wa mifugo | Matumizi bora ya Pembejeo | Usindikaji wa mazao | Uhifadhi na utunzaji wa mazingira | Matumizi ya zana bora za kilimo | Uboreshaji wa masoko ya mazao | Utunzaji wa nyuki | Utunzaji wa maji na uboreshaji wa udongo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Wilaya za awamu ya kwanza* | | | | | | | | | | |
| 1. Arumeru | 16 | 18 | 9 | 1 | 4 | 3 | 1 | 0 | 12 | 64 |
| 2. Hai | 7 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 17 |
| 3. Hanang | 12 | 15 | 17 | 0 | 5 | 14 | 2 | 0 | 15 | 80 |
| 4. Singida | 39 | 33 | 22 | 7 | 3 | 24 | 2 | 0 | 24 | 154 |
| 5. Morogoro | 24 | 24 | 7 | 1 | 2 | 5 | 1 | 1 | 8 | 73 |
| 6. Iringa | 16 | 8 | 18 | 0 | 0 | 6 | 0 | 0 | 10 | 58 |
| 7. Nachingwea | 29 | 21 | 14 | 6 | 0 | 4 | 18 | 0 | 8 | 100 |
| 8. Masasi | 20 | 43 | 3 | 7 | 1 | 21 | 18 | 0 | 3 | 116 |
| Jumla ndogo | 163 | 165 | 92 | 23 | 15 | 77 | 42 | 1 | 84 | 662 |
| *Wilaya za awamu ya pili* | | | | | | | | | | |
| 9. Iramba | 8 | 6 | 5 | 0 | 0 | 15 | 0 | 0 | 5 | 39 |
| 10. Urambo | 1 | 15 | 5 | 0 | 1 | 4 | 0 | 0 | 1 | 27 |
| 11. Uyui | 6 | 4 | 4 | 2 | 0 | 3 | 1 | 0 | 6 | 26 |
| 12. Sikonge | 14 | 7 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 5 | 31 |
| 13. Mbulu | 5 | 5 | 6 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 20 |
| 14. Karatu | 3 | 7 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 21 |
| 15. Kiteto | 10 | 11 | 7 | 1 | 1 | 10 | 0 | 0 | 4 | 44 |
| 16. Babati | 23 | 25 | 12 | 1 | 3 | 4 | 1 | 0 | 10 | 79 |
| 17. Zanzibar | 14 | 13 | 20 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 52 |
| Jumla ndogo | 84 | 93 | 67 | 7 | 7 | 37 | 5 | 0 | 39 | 339 |
| Jumla kuu | 247 | 258 | 159 | 30 | 22 | 114 | 47 | 1 | 123 | 1001 |
| % ya jumla | 24.7% | 25.8% | 15.9% | 3.0% | 2.2% | 11.4% | 4.7% | 0.1% | 12.3% | 100% |

*Kiambatisho Na. 3*

**SKIMU ZA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI NA MABWAWA ZILIZOENDELEZWA KATIKA MWAKA WA 2004/2005**

| **Skimu 17 zilizokzrabatiwa zenye jumla ya hekta 5100 ambazo zimekarabatiwa** | | | |
|---|---|---|---|
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| 1 | Nkenge | Bukoba | 40 |
| 2 | Ruhwiti | Kibondo | 200 |
| 3 | Mahurunga | Mtwara | 500 |
| 4 | Nkonkwa | Kigoma Vijijini | 100 |
| 5 | Kimwangamao | Moshi Vijijini | 1,200 |
| 6 | Mabungu | Moshi Vijijini | 450 |
| 7 | Ngage | Simanjiro | 450 |
| 8 | Misozwe | Muheza | 100 |
| 9 | Madizini | Kilosa | 100 |
| 10 | Sonjo | Kilombero | 100 |
| 11 | Kitaya | Mtwara | 300 |
| 12 | Kitanda | Namtumbo | 100 |
| 13 | Namatuhi | Songea | 100 |
| 14 | Muze/Sakolilo | Sumbawanga | 400 |
| 15 | Mangonyi | Singida | 200 |
| 16 | Magubike | Iringa Vijijini | 160 |
| 17 | Mbebe | Ileje | 400 |
| | | | 4,900 |
| Mabwawa matano (5) ambayo ambayo yamekarabatiwa | | | |
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| 1 | Ikowa | Dodoma Vijijini | 150 |
| 2 | Ruvu NAFCO | Kibaha | 100 |
| 3 | Mwangeza | Iramba | 152 |
| 4 | Maneke | Musoma | 200 |
| 5 | Kiseriani | Monduli | 30 |
| | **Mabwawa saba (7) ambayo yamesanifiwa** | | |
| 1 | Mkomazi | Korogwe | 200 |
| 2 | Tieme Masagi | Iramba | 200 |
| 3 | Kironda data 1 | Iramba | 100 |
| 4 | Usoke | Urambo | 100 |
| 5 | Nyaishozi | Karagwe | 50 |
| 6 | Mwele | Muheza | 100 |
| 7 | Choma cha Nkola | Igunga | 100 |
| | | | 1,482 |
| | | | |

| **Skimu zinazoendelezwa chini ya Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASPS). Za Irindi (hekta (610); Kilolo Utengule Usongwe Mbeya vijijini) (hekta 600)na Naming'ongo Mbozi (hekta 1,000) – Mbozi.** | | | |
|---|---|---|---|
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| 1 | Nyanzwa | Kilolo | 760 |
| 2 | Irindi | Kilolo | 610 |
| 3 | Utengule Usongwe | Mbeya Vijijini | 600 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | Ngaming'ongo | Mbozi | 1,000 |
| | | | 2,970 |
| **Skimu 10 za umwagiliaji maji mashambani zilizoainishwa na kubainishwa gharama zake za ujenzi, uendeshaji wa matengenezo** | | | |
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| 1 | Kinyope | Lindi | 200 |
| 2 | Pawaga | Iringa Vijijini | 2,000 |
| 3 | Mgongola | Morogoro Vijijini | 680 |
| 4 | Lower Moshi | Moshi Vijijini | 1,560 |
| 5 | Pamila | Kigoma Vijijini | 30 |
| 6 | Magoma | Korogwe | 200 |
| 7 | Luchili | Sengerema | 500 |
| 8 | Kisese | Mkuranga | 200 |
| 9 | Nkenge | Bukoba | 50 |
| 10 | Musa Mwinjanga | Hai | 646 |
| | | | |
| **Skimu za mfano 10 za umwagiliaji maji mashambani katika mwambao wa Ziwa Victoria wenye lengo la kuanzisha ukanda wa kijani kwa kutumia teknolojia rahisi za kupampu maji kutoka ziwani** | | | |
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| | | | |
| | Nyangwi | Nyamagana | 50 |
| | Nyashimba A | Ilemela | 40 |
| | Sangabuye | Ilemela | 55 |
| | Nyang'olongo | Ilemela | 60 |
| | Simuyu | Magu | 40 |
| | Mwamanyili | Magu | 40 |
| | Ilungu | Magu | 20 |
| | Lukungu | Magu | 20 |
| | Chabula | Magu | 30 |
| | Balili | Bunda | 60 |
| | | | 415 |

| **Skimu kumi zilizoendelezwa kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula (*Food Aid Counterpart Fund)*.** | | | |
|---|---|---|---|
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| | | | |
| 1 | Kikafu Chini | Hai | 200 |
| 2 | Mvumi | Kilosa | 200 |
| 3 | Mlali | Morogoro Vijijini | 80 |
| 4 | Chechami Mkoga | Iringa Vijijini | 180 |
| 5 | Shamwengo | MbeyaVijijini | 230 |
| 6 | Malolo | Nzega | 200 |
| 7 | Mkula | Kilombero | 250 |
| 8 | Ruaha Mbuyuni | Kililo | 300 |
| 9 | Lipwasi Ndorobo | Iringa | 250 |
| 10 | Nganjoni | Moshi Vijijini | 220 |
| | | | 2,110 |
| | | | |
| **Skimu zilizoendelezwa chini ya Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji** | | | |

| Mashambani (*PIDP*) | | | |
|---|---|---|---|
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| | | | |
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| | | | |
| 1 | Quash | Babati | 206 |
| 2 | Uhelela | Dodoma | 134 |
| 3 | Mpwayungu | Dodoma | 140 |
| 4 | Udimaa | Manyoni | 200 |
| 5 | Diomati | Mbulu | 373 |
| 6 | Harsha | Mbulu | 250 |
| 7 | Tumati | Mbulu | 112 |
| 8 | Sigili | Nzega | 329 |
| 9 | Chamipilu, | Nzega | 315 |
| 10 | Luhala | Kwimba | 160 |
| 11 | Nyambeho | Misungwi | 187 |
| 12 | Lakuyi | Misungwi | 92 |
| | | | 2,498 |
| | | | |

| Skimu zilizoendelezwa chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (*DADPs*) | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| S/N | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (HEKTA)** |
| 1 | Loiborsoil | Simanjiro | 100 |
| 2 | Lemkuna | Simanjiro | 100 |
| 3 | Ruvu Remit | Simanjiro | 100 |
| 4 | Ngaiti | Manyoni | 100 |
| 5 | Tlawi | Mbulu | 120 |
| 6 | Kisese | Kondoa | 55 |
| 7 | Kamanyanga | Manyoni | 50 |
| 8 | Gunge | Simanjiro | 300 |
| 9 | Msingi | Iramba | 100 |
| 10 | Mwashoma | Mbeya Vijijini | 80 |
| 11 | Kwala | Kibaha | 24 |
| 12 | Kidogozero | Bagamoyo | 24 |
| 13 | Ilonga | Kilosa | 80 |
| 14 | Kiroka | Morogoro ( R ) | 80 |
| 15 | Njagi | Kilombero | 100 |
| 16 | Msolwa | Kilosa | 90 |
| 17 | Makangaga | Kilwa | 100 |
| 18 | Kitere | Mtwara | 100 |
| 19 | Matekwe | Nachingwea | 100 |
| 20 | Mkoe Likuya | Ruangwa | 20 |
| 21 | Nangaramo | Masasi ( R ) | 150 |
| 22 | Likuyuseka | Songea | 100 |
| 23 | Nakahuga | Songea | 100 |
| 24 | Msanjesi | Songea | 100 |
| 25 | Kitanda | Songea | 100 |
| 26 | Fidia | Same | 500 |
| 27 | Marwa | Same | 200 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 28 | Kihurio | Same | 200 |
| 29 | Kigone Vunta | Same | 300 |
| 30 | Nangiriri | Hai | 100 |
| 31 | Kituri | Mwanga | 150 |
| 32 | Mkombozi | Mbozi | 400 |
| 33 | Ipungu | Mbozi | 100 |
| 34 | Iyendwe | Mbozi | 300 |
| 35 | Mbebe | Ileje | 200 |
| 36 | Mapongoro | Ileje | 150 |
| 37 | Ikumbiro Chitete | Ileje | 270 |
| 38 | Ifumbo | Chunya | 500 |
| 39 | Ngana | Kyela | 250 |
| 40 | Ilembo | Sumbawanga | 300 |
| 41 | Uruira | Mpanda | 400 |
| 42 | Igomaa | Mufindi | 120 |
| 43 | Itunundu | Iringa | 200 |
| 44 | Wanging'ombe | Njombe | 100 |
| 45 | Lifua | Ludewa | 100 |
| 46 | Kaning'ombe | Iringa ( R ) | 49 |
| 47 | Igigwa | Sikonge | 150 |
| 48 | Nyendera | Kibondo | 120 |
| 49 | Titye | Kasulu | 150 |
| 50 | Isuna | Nzega | 120 |
| 51 | Yava Yava | Mkuranga | 100 |
| 52 | Nholola | Shinyanga (V) | 145 |
| | | | 8,047 |

*Kiambatisho 4*

MBEGU MPYA ZILIZOTOLEWA NA TAASISI ZA UTAFITI ZILIZO CHINI YA WIZARA YA KILIMO MWAKA WA 2004/2005

| Kituo | Zao | Jina la mbegu | Sifa ya mbegu |
|---|---|---|---|
| Uyole | Mahindi | UH 6303 | • Inavumilia ugonjwa wa ukungu wa majani (Grey leaf spot)<br>• Ina uwezo wa kuzaa tani 10 kwa hekta |
| | | Uyole 04 | • Inavumilia ugonjwa wa kutu na anthracnose<br>• Inazaa tani 3 kwa hekta |
| | Maharage | BILFA | • Ina rangi nyekundu yenye madoa madoa meupe<br>• Inavumilia magonjwa<br>• Inatoa tani 2.5 kwa hekta |
| | Ngano | SIFA | • Inazaa tani 5 kwa hekta<br>• Ina sifa nzuri kwa ajili ya uokaji<br>• Inavumilia magonjwa kama ukungu |
| Kibaha | Muhogo | Kiroba | • Inavumilia ugonjwa wa *mosaic* na magonjwa mengine<br>• Inazaa tani 27 kwa hekta<br>• Inaweza kukaa muda mferu bila kuvunwa na isiharibike |
| | | Hombolo 95 | • Ina uwezo wa kuzaa tani 18 kwa kekta<br>• Inakaa siku nne bila kuharibika baada ya kuvunwa (kuchimbwa). |

*Kiambatisho 5*

**VITUO VYA WANYAMAKAZI VILIVYOFANYIWA UKARABATI MWAKA WA FEDHA 2002/2003**

| S/NA. | KITUO | WILAYA | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kate | Nkasi | 4,000,000 |
| 2.. | Mwese | Mpanda | 4,000,000 |
| 3. | Inyala | Mbeya (v) | 9,000,000 |
| 4. | Rujewe | Mbarali | 9,000,000 |
| 5. | Mallya | Kwimba | 7,000,000 |
| 6. | Negezi | Shinyanga | 4,000,000 |
| 7. | Tarime | Tarime | 7,000,000 |
| 8. | Gairo | Kilosa | 4,000,000 |
| 9. | Ibologero | Igunga | 4,000,000 |
| 10. | Chikola | Manyoni | 4,000,000 |
| 11. | Bihawana | Dodoma | 9,000,000 |
| 12. | Chamkoroma | Kongwa | 4,000,000 |
| 13. | Babati | Babati | 6,000,000 |
| 14. | Mayale | Njombe | 7,000,000 |
| 15. | Ilambilole | Iringa | 7,000,000 |
| 16. | Nyololo | Mufindi | 7,000,000 |
| 17. | Korogwe | Korogwe | 7,000,000 |
| 18. | Lugoba | Bagamoyo | 4,000,000 |
| 19. | Chipuputa | Mtwara | 4,000,000 |
| 20. | Uru chini | Moshi (v) | 4,000,000 |
| 21. | Libambo | Songea | 10,000,000 |
| **JUMLA** | | | 125,000,000 |

**VITUO VYA WANYAMAKAZI VILIVYOFANYIWA UKARABATI MWAKA WA FEDHA 2003/2004**

| S/NA. | KITUO | WILAYA | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kisesa | Mufindi | 5,000,000 |
| 2. | Kitowo | Iringa (v) | 5,000,000 |
| 3. | Masimbwe | Ludewa | 3,000,000 |
| 4. | Mapogoro | Ileje | 8,000,000 |
| 5. | Rujewa | Mbarali | 4,000,000 |
| 6. | Kishinda | Sengerema | 5,000,000 |
| 7. | Msangano | Mbozi | 8,000,000 |
| 8. | Milama | Mvomero | 7,000,000 |
| 9. | Gairo | Kilosa | 2,000,000 |
| 10. | Inonelwa | Misungwi | 8,000,000 |
| 11. | Upuge | Uyui | 10,000,000 |
| 12. | Ibologera | Igunga | 3,000,000 |
| 13. | Urambo | Urambo | 6,000,000 |
| 14. | Mwamapalala | Bariadi | 5,000,000 |
| 15. | Mwankoko | Singida (M) | 7,097,623 |
| 16. | Mtawanya | Mtwara (v) | 4,650,000 |
| 17. | Ilongero | Singida (v) | 4,000,000 |
| 18. | Ikungi | Singida (v) | 7,000,000 |
| 19. | Bangayega | Manyoni | 5,500,000 |
| 20. | Mukulu | Iramba | 6,000,000 |
| 21. | Chigulwe | Geita | 3,000,000 |
| 22. | Kivingo | Lushoto | 4,000,000 |
| 23. | Kate | Nkasi | 4,000,000 |
| 24. | Mwanhala | Nzega | 6,000,000 |
| 25. | Burunga | Serengeti | 5,000,000 |
| 26. | Buhemba | Musoma | 5,000,000 |
| 27. | MATI – Mtwara | Mtwara | 2,000,000 |
| 28. | MATI – Igurusi | Mbeya (v) | 4,000,000 |
| 29. | MATI – Mlingano | Muheza | 2,000,000 |
| 30. | MATI – Ukiriguru | Misungwi | 2,000,000 |
| 31. | MATI- Uyole | Mbeya (v) | 2,500,000 |
| 32. | MATI Mtwara | Mtwara | 2,000,000 |
| 33. | KATC - Moshi | Moshi (v) | 2,000,000 |
| | **JUMLA** | | 156,747,623 |

VITUO VYA WANYAMAKAZI VILIVYOFANYIWA UKARABATI
MWAKA WA FEDHA 2004/2005

| S/NA. | **KITUO** | WILAYA | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1. | Lyasa | Kilolo | 7,000,000 |
| 2. | Kisilo | Njombe | 7,000,000 |
| 3. | Masimbwe | Ludewa | 1,500,000 |
| 4. | Luana | Ludewa | 4,000,000 |
| 5. | Mapogoro | Ileje | 3,250,000 |
| 6. | Ipinda | Kyela | 8,000,000 |
| 7. | Kisangwa | Bunda | 5,000,000 |
| 8. | Pongwe | Tanga | 7,000,000 |
| 9. | Milama | Mvomero | 4,000,000 |
| 10. | Tabora | Kipalapala | 7,000,000 |
| 11. | Upuge | Uyui | 1,500,000 |
| 12. | Mwankoko | Singida (M) | 3,000,000 |
| 13. | Mtawanya/Lilingu | Mtwara (V) | 5,000,000 |
| 14. | Ilongero | Singida (V) | 4,000,000 |
| 15. | Ikungi | Singida (V) | 4,000,000 |
| 16. | Bangayega | Manyoni | 2,000,000 |
| 17. | Mukulu | Iramba | 5,000,000 |
| 18. | Kabila | Magu | 7,000,000 |
| 19. | Kivingo | Lushoto | 5,000,000 |
| 20. | Kibakwe | Mpwapwa | 8,000,000 |
| 21. | Utiri | Mbinga | 8,000,000 |
| 22. | Rubambagwe | Biharamulo | 5,000,000 |
| 23. | Malagarasi | Kigoma | 4,500,000 |
| | | JUMLA | 115,750,000 |

*Kiambatisho 6*

KIASI CHA FEDHA ZILIZOTOLEWA NA MFUKO WA TAIFA WA PEMBEJEO ZA KILIMO KUANZIA 2002/2003 HADI TAREHE 12 APRILI, 2005.

| Benki | Mikopo Iliyotolewa (Tsh) | Kiasi kilichorejeshwa (Tsh) |
|---|---|---|
| Kilimanjaro Coop. Bank | | |
| 2002/2003 | 103,000,000.00 | 103,000,000.00 |
| EXIM Bank | | |
| 2002/2003 | 1,902,100,000 | 1,452,678,571 |
| 2003/2004 | 908,244,000 | 363,452,805 |
| 2004/2005 | 1,235,800,000 | 100,925,926 |
| Mufindi Community Bank | | |
| 2003/2004 | 592,500,000 | 280,994,643 |
| Kagera Coop. Bank | | |
| 2003/2004 | 278,450,000 | 183,725,214 |
| 2004/2005 | 20,000,000 | |
| SCCULT(1992) LTD. | | |
| 2003/2004 | 1,753,830,000 | 997,514,033 |
| 2004/2005 | 900,000,000 | - |
| Mbinga Community Bank | | |
| 2004/2005 | 299,004,300 | 31,333,766 |
| Mfuko wa Pembejeo | | |
| • Kukarabati trekta | | |
| 2003/2004 | 351,522,000 | 46,057,946 |
| 2004/2005 | 387,639,200 | 11,472,222 |
| • Trekta Mpya | | |
| 2003/2004 | 113,731,178.00 | - |
| 2004/2005 | 200,000,000.00 | 1,690,429 |
| • Mikopo ya pembejeo | | |
| 2004/2005 | 630,932,200.00 | 10,000,000 |
| Akiba Commercial Bank | | |
| 2004/2005 | 21,650,000 | - |
| CF Union Bank | | |
| 2004/2005 | 75,000,000.00 | - |
| **Jumla** | **9,773,452,878** | **3,584,799,811** |

**Chanzo: Mfuko wa Pembejeo 2005**

*Kiambatisho 7*

TAARIFA YA IDADI YA WANAFUNZI WALIOPO VYUONI

| S/N | CHUO | Mwaka wa kwanza | | Mwaka wa Pili | | Jumla | | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mke | Mme | Mke | Mme | Mke | Mme | |
| 1 | Uyole | 29 | 118 | 16 | 48 | 45 | 166 | 211 |
| 2 | Ukiriguru | 12 | 61 | 12 | 23 | 24 | 84 | 108 |
| 3 | Ilonga | 37 | 49 | 5 | 14 | 42 | 63 | 105 |
| 4 | Mlingano | - | 22 | - | 20 | - | 42 | 42 |
| 5 | Igurusi | 1 | 23 | 2 | 16 | 3 | 38 | 41 |
| 6 | Tumbi | 7 | 21 | 4 | 15 | 11 | 36 | 47 |
| 7 | Mtwara | 10 | 29 | 4 | 2 | 14 | 31 | 45 |
| 8 | NSI - Kidatu | 23 | 222 | - | - | 24 | 221 | 245 |
| JUMLA | | 120 | 543 | 43 | 138 | 163 | 681 | 844 |

***Kiambatisho 8***

IDADI ZA AINA ZA MIFUGO WANAOTUMIWA KATIKA MAFUNZO YA VITENDO KATIKA VYUO VYA MAFUNZO YA KILIMO VYA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA KATIKA MWAKA 2004/2005

| SN | CHUO | AINA YA MIFUGO | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ng'ombe | Kuku | Mbuzi | Kondoo | Punda | Nguruwe | Maksai |
| 1. | Uyole | 41 | 592 | 11 | 11 | 6 | 16 | 8 |
| 2. | Ilonga | 92 | 231 | 29 | 71 | 5 | 25 | 6 |
| 3. | Ukiriguru | 38 | 617 | 9 | 5 | 6 | 70 | 4 |
| 4. | Mlingano | 28 | 150 | - | - | 8 | - | 4 |
| 5. | Mtwara | 17 | 178 | - | - | - | 22 | 4 |
| | Jumla | 216 | 1,768 | 49 | 87 | 25 | 133 | 26 |

*Kiambatisho 9*

IDADI YA WAKULIMA WALIOPATA MAFUNZO KATIKA FANI MBALIMBALII ZA **KILIMO KATIKA VYUO VYA MAFUNZO YA KILIMO VYA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA** MWAKA WA 2004/2005

| SN | CHUO | IDADI YA WAKULIMA WALIOFUNDISHWA | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mke | Mme | Jumla | Gharama za mafunzo |
| 1 | UYOLE | 244 | 763 | 1007 | 95,096,675 |
| 2 | UKIRIGURU | 120 | 194 | 314 | 9,318,500 |
| 3 | ILONGA | 20 | 21 | 4 | 74,000 |
| 4 | MLINGANO | 237 | 391 | 628 | 6,782,500 |
| 5 | IGURUSI | 2,164 | 2,486 | 4,650 | Out reach Activities |
| 6 | TUMBI | - | - | - | - |
| 7 | MTWARA | 144 | 144 | 288 | 13,441,000 |
| 8 | KATC | 981 | | | |
| 9 | NSI KIDATU | 43 | 137 | 180 | Out reach activities |
| | JUMLA | 3,953 | 4,796 | 8,749 | 233,583,720 |

*Kiambatisho 10*

MAENEO YA KAZI YA UTAFITI WA MAZAO KATIKA VITUO VYA UTAFITI VYA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA KWA MWAKA WA 2005/06

| Kanda | Tathmini ya mbegu za mazao | Uzalishaji wa vipando na mbegu | Maonyesho ya usindikaji | Uzalishaji mbegu mam za msingi | Utafiti wa mazao ya viungo na mboga mboga | Tathmini ya mbinu bora za kilimo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Magharibi | Tumbi (maharage, mahindi, mpunga, michikichi, karanga,alizeti | - | - | Michikichi | - | Mpunga, muhogo, mahindi |
| Mashariki | Ilonga: mahindi, mtama, mikunde,alizeti<br>Ifakara:Mpunga<br>Dakawa: Mpunga<br>Mlingano: Mkonge<br>Kibaha: Muhogo, Miwa<br>Mikocheni: Minazi | Kibaha: Muhogo, viazi vitamu<br>Mlingano: Mkonge<br>Ilonga: Pamba<br>Ifakara na Dakawa: Mpunga | Ilonga: Mbaazi<br>Kibaha: Muhogo | Ilonga: Mahindi, mtama, uwele, kunde<br>Ifakara: Mpunga<br>Dakawa: Mpunga | Ifakara: Viungo | Mikocheni: Minazi<br>Mlingano: Mkonge<br>Ilonga: Mikunde |
| Kaskazini | Seliani: Mahindi, ngano, Maharage<br>Tengeru: Mboga, Matunda, Viungo, Migomba | Seliani: Ngano, Mahindi<br>Tengeru: Migomba, Mboga mboga | - | Seliani: Ngano, Mahindi<br>Tengeru: Migomba, Mboga mboga | Tengeru: Viungo, Matunda, Mboga mboga | Seliani: Mahindi, Maharage |
| Kati | Hombolo: Mtama, Uwele, Muhogo<br>Makutupora: Zabibu | - | Hombolo: Muhogo<br>Makutupora: Alizeti | - | - | Makutupora: Alizeti |
| Kusini | Naliendele: Karanga, Ufuta,Muhogo, Mtama, korosho<br>Mkumba: Muhogo, Kunde, korosho | Naliendele: Korosho, Muhogo | Naliendele: Muhogo | Naliendele: Ufuta, karanga, Korosho | - | - |
| Nyanda za juu Kusini | Uyole: Mahindi, Soya, Ngano, Maharage, Viazi mviringo, Pareto | Uyole: Pareto, Viazi mviringo, Pareto, Mahindi, Maharage, Soya | Uyole: Soya | Uyole: Mahindi, Maharage, Ngano, Viazi mviringo, Pareto | Uyole: Viungo, Matunda | Uyole: Mahindi, Viazi mviringo |
| Ziwa | Ukiriguru: Mahindi, Mtama, Muhogo, Viazi vitamu, pamba<br>Maruku: Migomba, Viungo | Ukiriguru: Muhogo, Viazi vitamu Pamba<br>Maruku: Migomba, | - | Ukiriguru: Muhogo, Viazi vitamu Pamba<br>Maruku: Migomba, | Maruku: Viungo | Maruku: Migomba, |

*Kiambatisho 11*

SKIMU ZA UMWAGILIAJI MASHAMBANI NA MAMABWAWA YATAKAYOENDELEZWA MWAKA WA 2005/2006

| **S/NA.** | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (ha)** |
|---|---|---|---|
| 1. | PAWAGA | IRINGA (V) | 500* |
| 2. | MBEBE | ILEJE | 540 |
| 3. | IFUMBO | CHUNYA | 300* |
| 4. | NAMING'ONGO | MBOZI | 1,000* |
| 5. | MANG'ONYI | MANYONI | 400* |
| 6. | IKOWA | DODOMA (V) | 300 |
| 7. | MIBONO/CHABUTWA | SIKONGE | 500 |
| 8. | NKONKWA | KIGOMA (V) | 300* |
| 9. | MKUTI | KIGOMA (V) | 100* |
| 10. | KATUNGURU | SENGEREMA | 50 |
| 11. | KATENGERA | KIBONDO | 300* |
| 12. | KINYOPE | LINDI (V) | 350 |
| 13. | LITUMBANDYOSI | MBINGA | 120* |
| 14. | LUNDO | MBINGA | 400* |
| 15. | LIYUNI | NAMTUMBO | 400* |
| 16. | SELELA | MONDULI | 350 |
| 17. | MAKORORA | KOROGWE | 250* |
| 18. | MUSA MWINJANGA | HAI | 676 |
| 19. | MBUGUNI SHANGO | ARUMERU | 650 |
| 20. | MVUMI | KILOSA | 293 |
| 21. | MADIZINI | KILOSA | 132 |
| 22. | KISERE | MKURANGA | 200* |
| 23. | SONJO | KILOMBERO | 200* |
| 24. | IRIENYI | TARIME | 60 |
| 25. | CHIRORWE | MUSOMA | 40 |
| 26. | NANSIMO | BUNDA | 50 |
| 27. | CHERECHE | TARIME | 80 |
| 28. | OCHUNA | TARIME | 50 |
| 29. | BIGOMBO VALLEY | NGARA | 100 |
| 30. | NAMBECHA | NAMTUMBO | 400 |
| **JUMLA** | | | **9,491** |

*Ujenzi wa skimu hii utaongeza eneo linalomwagiliwa maji mashambani wakati skimu zilizobaki zitachangia ongezeko la uzalishaji zaidi ya msimu moja (*increased cropping* ***intensity***)

SKIMU ZITAKAZOTEKELEZWA CHINI YA MPANGO HUSISHI WA KUENDELEZA UMWAGILIAJI KATIKA MAENEO YENYE UKAME (*PIDP*) MWAKA WA 2005/2006

| S/NA. | SKIMU | WILAYA | ENEO (ha) |
|---|---|---|---|
| 1. | IYUWA | MPWAPWA | 170 |
| 2. | MASIMBA | IRAMBA | 400 |
| 3. | MLANDALA | IRAMBA | 300 |
| 4. | DONGOBESH | MBULU | 200 |
| 5. | GUWANG | MBULU | 110 |
| 6. | IJINGA | MASWA | 360 |
| 7. | ILUJAMATE | MISUNGWI | 200 |
| 8. | NYASHIDALA | MISUNGWI | 370 |
| 9. | BUYUBI | MASWA | 311 |
| 10. | MISWAKI/BUHEKELA | IGUNGA | 450 |
| **JUMLA** | | | **2,871** |

MABWAWA YATAKAYOJENGWA MWAKA WA 2005/2006

| S/NA. | SKIMU | WILAYA | ENEO (ha) |
|---|---|---|---|
| 1. | MWANGEZA | IRAMBA | 193 |
| 2. | MASINONO | MUSOMA | 50 |
| 3. | MESAGA | SERENGETI | 50 |
| 4. | NKINIZIWA | NZEGA | 220 |
| 5. | USOKE | URAMBO | 391 |
| 6. | ISIKIZYA | UYUI | 121 |
| 7. | MISOZWE | MUHEZA | 100 |
| 8. | MWELE | MUHEZA | 35 |
| 9. | MSIMBA | KILOSA | 500 |
| 10. | NYANG'OLO | BAGAMOYO | 40 |
| **JUMLA** | | | **1,700** |

MASHAMBA YA MBEGU YATAKAYOENDELEZWA MIUNDOMBINU YA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI MWAKA WA 2005/2006

| S/NA. | SKIMU | WILAYA | ENEO (ha) |
|---|---|---|---|
| 1. | DABAGA SEED FARM | IRINGA | 200 |
| 2. | ARUSHA SEED FARM | ARUSHA | 80 |
| **JUMLA** | | | **280** |

MAENEO YATAKAYOENDELEZWA KATIKA SKIMU ZA MFANO ILI KUANZISHA UKANDA WA KIJANI KATIKA MWAMBAO WA ZIWA VIKTORIA NA ZIWA NYASA MWAKA WA 2005/2006

| S/NA. | SKIMU | MKOA | ENEO (ha) |
|---|---|---|---|
| 1. | ZIWA VIKTORIA | MWANZA | 100 |
| 2. | ZIWA NYASA | RUVUMA | 100 |
| **JUMLA** | | | **200** |

SKIMU ZITAKAZOTEKELEZWA KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA PAMOJA WA TANZANIA NA JAPAN WA MSAADA WA CHAKULA (*FOOD AID COUNTERPART FUND*) MWAKA WA 2005/2006

| **S/NA.** | **SKIMU** | **WILAYA** | **ENEO (ha)** |
|---|---|---|---|
| 1. | BUGORORA | BUKOBA | 100 |
| 2. | RWANG'EENYI | TARIME | 100 |
| 3. | LAWATE KISANGARA | HAI | 250 |
| 4. | MSHINDO LUMECHA | NAMTUMBO | 300 |
| 5. | KIWERE | IRINGA (V) | 300 |
| 6. | BUGUGA | KIBONDO | 200 |
| 7. | WAMI LUHINDO | MVOMERO | 200 |
| **JUMLA** | | | **1,350** |

## *Kiambatisho 12*

Mgawanyo wa fedha kwa mwaka wa 2005/2006 umezingatia utekelezaji wa maeneo makuu ya kipaumbele kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA kama ifuatavyo:-

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | Umwagiliaji Maji Mashambani | - | **shilingi bilioni** | **8.3** |
| 2. | Ununuzi wa Nafaka (SGR) | - | **shilingi bilioni** | **8.2** |
| 3. | Ruzuku ya mbolea na madawa ya korosho | - | **shilingi bilioni** | **8.0** |
| 4. | Ruzuku kwa Mashirika na Asasi zilizo chini ya Wizara | - | **shilingi bilioni** | **5.6** |
| 5. | Huduma za Utafiti wa Mazao | - | **shilingi bilioni** | **4.0** |
| 6. | Mfuko wa Pembejeo | - | **shilingi bilioni** | **3.9** |
| 7. | Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea- | - | **shilingi bilioni** | **2.0** |
| 8. | Ruzuku kwa Mashirika ya Nje | - | **shilingi bilioni** | **1.2** |
| 9. | Huduma za ugani | - | s**hilingi bilioni** | **1.0** |

Mgawanyo wa fedha kwa kila idara ni kama ifuatavyo:

**(i) Kifungu 1001: UTAWALA NA UTUMISHI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - Mishahara | - | **shilingi bilioni** | **0.285** |
| - Utawala | - | **shilingi bilioni** | **1.969** |
| - Sheria (legal Unit) | - | **shilingi bilioni** | **0.032** |
| - Habari | - | **shilingi bilioni** | **0.030** |
| **Jumla Utawala na Utumishi** | **-** | **shilingi bilioni** | **2.216** |

**(ii) Kifungu 1002: UHASIBU NA FEDHA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - Mishahara | - | **shilingi bilioni** | **0.129** |
| - Uhasibu | - | **shilingi bilioni** | **0.219** |
| - Ukaguzi wa ndani | **-** | **shilingi bilioni** | **0.100** |
| **Jumla ya kifungu 1002** | **-** | **shilingi bilioni** | **0.448** |

**(iii) Kifungu 1003: SERA NA MIPANGO**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **-** Mishahara | - | **shilingi bilioni** | **0.167** | |
| **-** Mipango na bajeti | - | **shilingi bilioni** | **0.281** | |
| **-** Takwimu | **-** | **shilingi bilioni** | **0.260** | **-** |
| **-** Uchambuzi wa sera | - | **shilingi bilioni** | **0.074** | **-** |
| **-** Usimamizi wa Idara | - | **shilingi bilioni** | **0.156** | |
| - Uratibu wa ASDP | - | **shilingi bilioni** | **0.550** | |

- **Jumla ya kifungu 1003 - shilingi bilioni 1.489**

**(iv) Kifungu 2001: IDARA YA MAENDELEO YA MAZAO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mishara | - | **shilingi bilioni** | **1.539** |
| Ruzuku ya mbolea na madawa | - | **shilingi bilioni** | **8.000** |
| - Udhibiti wa Visumbufu vya mimea | - | **shilingi bilioni** | **1.980** |
| - Huduma za ugani | - | **shilingi bilioni** | **1.000** |
| - Kuzalisha mbegu bora za mazao | - | **shilingi bilioni** | **0.500** |
| - Uendelezaji wa mazao mapya | - | **shilingi bilioni** | **0.400** |
| - Ruzuku kwa mashirika ya nje (FAO, IFAD, DLCO-EA, IRLCO-CSA, ISTA, International Society for Horticultural services) | - | **shilingi bilioni** | **1.127** |
| - Ruzuku kwa mashirika ya ndani | - | **shilingi bilioni** | **3.823** |
| - Usimamizi wa Idara | - | **shilingi bilioni** | **0.330** |

**MFUKO WA PEMBEJEO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - Mikopo ya pembejeo | - | **shilingi bilioni** | **1.900** |
| - Mikopo ya matrekta | - | **shilingi bilioni** | **1.380** |
| - Mikopo ya zana | - | **shilingi bilioni** | **0.222** |
| - Usimamizi wa mfuko | - | **shilingi bilioni** | **0.390** |
| **JUMLA YA KIFUNGU 2001:** | - | **shilingi bilioni** | **22.592** |

**(v) Kifungu 2002: IDARA YA UFUNDI NA UMWAGILIAJI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| - Mishahara | - | **shilingi bilioni** | **0.358** |
| - Umwagiliaji maji mashambani | - | **shilingi bilioni** | **8.300** |
| - Zana za kilimo | - | **shilingi bilioni** | **0.900** |
| - Hifadhi ya Ardhi | - | **shilingi bilioni** | **0.400** |
| - Usimamizi wa Idara | - | **shilingi bilioni** | **0.141** |
| **Jumla ya kifungu 2002** | - | **shilingi bilioni** | **10.099** |

**(vi) Kifungu 3001: UTAFITI NA MAFUNZO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mishahara | - | **shilingi bilioni** | **2.660** |
| - Huduma za utafiti wa mazao | - | **shilingi bilioni** | **2.813** |
| - Huduma za mafunzo | - | **shilingi bilioni** | **0.709** |
| - Usimamizi wa idara | - | **shilingi bilioni** | **0.479** |
| - Ruzuku kwa mashirika ya ndani | - | **shilingi bilioni** | **1.835** |

- Ruzuku kwa mashirika ya nje - **shilingi bilioni** **0.049**
  (CABI, SADC/SACCAR, SADC/Genetic Resource)
- **Jumla ya kifungu 3001 - shilingi bilioni 8.545**

**(vii) Kifungu 5001: IDARA YA USALAMA WA CHAKULA**

- Mishahara - **shilingibilioni 0.089**
- Hifadhi ya Chakula ngazi ya kaya - **shilingi bilioni 0.450**
- Tahadhari ya awali (Early warning) - **shilingi bilioni 0.204**
- Usimamizi wa Idara - **shilingi bilioni 0.153**

**Jumla ya kifungu 5001 - shilingi bilioni 0.896**

**(viii) Kifungu 5002: HIFADHI YA CHAKULA CHA TAIFA**

- Mishahara **-** **shilingi bilioni 0.123**
- Ununuzi wa nafaka - **shilingi bilioni 8.000**
- Usimamizi wa Idara - **shilingi bilioni 0.225**
- **Jumla ya kifungu 5002 - shilingi bilioni 8.348**

**BAJETI YA MAENDELEO**

| MRADI | 2005/2006 | | |
|---|---|---|---|
| | **Fedha za ndani (Shs. bilioni)** | **Fedha za nje (Shs. bilioni)** | **Jumla (Shs. bilioni)** |
| **Kifungu 1001: Utawala na Utumishi** | | | |
| Tanzania Multi-Sectoral AIDS Project (TMAP) | | **0.100** | **0.100** |
| **Jumla ya Kifungu(1001)** | | **0.100** | **0.100** |
| **Kifungu 1003: Sera na Mipango** | | | |
| Agriculture Sector Programme Support (ASPS II) | 0.100 | 3.000 | 3.100 |
| Agriculture Sector Development Programme (ASDP) | 4.500 | | 4.500 |
| District Agricultural Investment Project (DASIP) | 0.470 | 4.000 | 4.470 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jumla ya Kifungu(1003)** | **5.070** | **7.000** | **12.070** |
| ***Kifungu 1004: Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo*** | | | |
| *Agriculture Training Institutes* | 0.265 | 0.291 | 0.556 |
| **Jumla ya Kifungu (1004)** | **0.265** | **0.291** | **0.556** |
| Kifungu 2001:Maendeleo ya Mazao | | | |
| Lake Victoria Environmental Mgt. Project (LVEMP) | 0.100 | | 0.100 |
| Participatory Agriculture Dev. And Empowerment Programme (PADEP) | 0.454 | 9.541 | 9.996 |
| Special Programme for Food Security (SPFS) | 0.100 | 0.060 | 0.160 |
| **Jumla ya Kifungu(2001)** | **0.654** | **9.601** | **10.256** |
| ***Kifungu 2002: Huduma za Umwagiliaji na Ufundi*** | | | |
| Participatory Irrigation Dev. Programme (PIDP) | 0.450 | 2.239 | 2.690 |
| River Basin Mgt. and Smallholder Irrigation Improvement Project (RBM-SIIP) | 0.200 | | 0.200 |
| Soil and Water Conservation | 0.070 | | 0.070 |
| **Jumla ya Kifungu(2002)** | **0.720** | **2.239** | **2.960** |
| Kifungu 3001: Utafiti na Mafunzo | | | |
| Agriculture Service Support Programme (ASSP) | 0.159 | 27.919 | 28.079 |
| Tanzania Agric. Research Project (TARP II) | 0.571 | | 0.571 |
| Stabex Coffee | | 8.050 | 8.050 |
| East Zone Client Oriented Research & Extension | | 0.827 | 0.827 |
| ***Jumla ya Kifungu(3001)*** | **0.995** | **37.087** | **38.083** |
| **JUMLA** | **7.440** | **56.050** | **63.490** |

**JUMLA YA FUNGU 43 Shilingi Bilioni 118.124**